# Nipashe

Jumanne Julai 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580277

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN

215779502




RIPOTI MAALUM

## Jumuiya Hifadhi Barunge yajiendesha mfano wa serikali, bajeti ya mabilioni

UKURASA 4

# Membe anawa mikono CCM



**AREJESHA** kadi ya uanachama, amwarifu rasmi Dk. Bashiru, ashukuru kwa yote aliyotendewa... *Endelea ukurasa 2*



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akionyesha kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, masanduku ya pesa Sh. bilioni 2.8 mali ya benki ya NMB, zinazodaiwa kutoroshwa na watu 32 wakiwamo wafanyakazi watano wa kampuni ya ulinzi ya Security Group of Africa maarufu (SGA). **Habari Uk. 3**. PICHA: JUMANNE JUMA

## BAA LA CORONA



'Usichukulie poa unategemewa'

* **Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka**
* **Kaa kwa kuachiana nafari hatua 2 au 3**
* **Vaa barakoa**
* **Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo**

## WALIMU WADAIWA KUUZA JINA LA MWANAFUNZI

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Magufuli asema ruksa wateule wake kutafuta riziki kwingine



UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA, NAMUNGO WAKATI UTAONGEA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Membe anawa mikono CCM

**Na Joseph Mwendapole**

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wakati wa utawala wa awamu ya nne, Bernard Membe, amerejesha kadi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Membe (66), alikabidhi kadi hiyo jana katika Kijiji cha Rondo mkoani Lindi, akisindikizwa na mke wake pamoja na baadhi ya wananchi wa kijiji hicho.

"Nimemwandikia Katibu Mkuu wa CCM (Dk. Bashiru Ally) kuhusu tukio hili na kukishukuru chama kwa mema kilichonitendea. Ninawatakia kila la heri viongozi na wanachama wote," Membe aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter muda mfupi baada ya kukabidhi kadi hiyo.

Juzi, Membe alizungumza na mwandishi mkongwe nchini, Jenerali Ulimwengu, akiahidi kurudisha kadi hiyo kama ishara ya kujitoa rasmi kwenye chama hicho tawala.

Alisema amefukuzwa na chama chake kwa madai ya utovu wa nidhamu, hivyo itakapofika Julai sita (jana) Jumatatu, atarejesha kadi kwa wenyewe, ili wajue kwamba ameshajitoa rasmi.

"Ni kweli nilifukuzwa kwenye chama changu na ninaomba nitumie fursa hii kuutangazia umma kuwa siku ya Jumatatu Julai 6 nitarejesha rasmi kadi ya CCM kwa wenyewe," Membe alisema wakati akijibu swali aliloulizwa na Ulimwengu.

Februari 28 mwaka huu, CCM ilitangaza kuwa Kamati Kuu ya chama hicho imemvua uanachama Membe baada ya kuhojiwa na Kamati ya Maadili na Usalama ya chama hicho.

Kamati hiyo inayoongozwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Phillip Mangula, ilimhoji Membe kwa saa tano kwenye ofisi za makao makuu ya chama hicho mkoani Dodoma Februari 6 mwaka huu.

Mbali na Membe, makada wengine wa CCM waliohojiwa kwa nyakati tofauti ni makatibu wakuu wastaafu, Abdulahman Kinana na Yusuf Makamba, ambao chama kiliwapa onyo na kuwasamehe baada ya kuomba msamaha.

Baada ya kutoka kuhojiwa, Membe alisema safari ya kwenda Dodoma ilikuwa na manufaa makubwa kwake, kwa chama na kwa taifa zima.

# JPM asema ruksa wateule kuondoka

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS John Magufuli amewataka viongozi anaowateua kushika nafasi mbalimbali kuridhika na wanachokipata, huku akisisitiza kuwa watakaohitaji kwenda kuwatumikia wananchi kwenye maeneo mengine wanaruhusiwa.

Kauli hiyo aliitoa jana Ikulu jijini hapa alipokuwa akizungumza baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni.

Rais alisema hayo jana kutokana na baadhi ya wateule wake kutajwa kuwa wanakwenda katika majimbo ya uchaguzi kwa ajili ya kuwania kuteuliwa kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Alisema kuna baadhi ya wateule wake wamekuwa wakimwomba ruhusa na amekuwa akitoa haraka sana, huku akisema matatizo ya wananchi hayawezi kuwasubiri wao warudi.

Hata hivyo, aliwataka wateule hao kila mmoja kuridhika na alichopata kwa kuwa ni kitu kizuri.

"Mkaridhike na mlichopata kwa kuwa kuridhika nako ni kitu kizuri. Hata mfano wa Yesu inawezekana si mzuri sana hapa, wale waliopewa talanta hawakupewa zilizolingana. Mwingine alipewa 10, mwingine alipewa moja, lakini kinachotakiwa tukaridhike na hizi talanta tulizopewa tukazizalishe zaidi," alisema huku akisisitiza kuwa kuzizalisha kwao talanta hizo ni kuwatumikia Watanzania watakaokuwa wanawaongoza.

"Hicho ndicho ninachowaomba sana. Kwa hiyo yeyote anayejisikia kuniomba ruhusa hata leo mniombe tu mimi nitatoa. Nina Ma-DAS (Katibu Tawala Wilaya) watatu nikitoka hapa naenda kuwapa ruksa. Nafikiri ni DAS wa Gairo na Malinyi, nafikiri ruksa zao ninaziandaa waende. Kila anayetaka kuomba mimi nitampa," alisema.

Alisema akiwanyima ruhusa atakuwa amefanya dhambi mbaya kwa hiyo alitoa ruhusa kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ili waende huko kwingine kuzuri.

"Ninawaamini kwa kazi kubwa mnayofanya. Huyu aliyeenda Same alikuwa Ofisa Mipango Arusha, nilipoombwa ruksa na yule wa Same mtoto wa Dk. (William) Shija (marehemu) nikampa haraka haraka ili kazi ziendelee, taifa hili lazima liendelee," alisema.



**BANGI YAPONZA VIGOGO**

RAIS Magufuli aliagiza kuondolewa mamlaka na kushushwa vyeo Mkuu wa Polisi (OCD), Ofisa Usalama (DsO), Mkuu wa Upelelezi (OCCID) wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha kutokana na kushindwa kudhibiti kilimo cha bangi.

Sambamba na hilo, amemthibitisha aliyekuwa Kaimu Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, James Kaji, kuwa Kamishna Jenerali wa mamlaka hiyo, baada kuridhishwa na utendaji kazi wake katika kupambana na dawa za kulevya, ikiwamo operesheni ya kukamata wanaolima bangi wilayani Meru.

Alisema ni vigumu kuwavumilia viongozi hao wa vyombo vya usalama kwa kamishna huyo kutoka Dodoma kwenda kukamata bangi wilayani Meru ilhali kuna viongozi kwenye wilaya hiyo.

"Ninawapongeza viongozi wengine ambao nimeshirikiana nanyi, vyombo vya ulinzi na usalama mmefanya kazi kubwa sana. Jana nilikuona wa dawa za kulevya ukienda kwenye milima kule na watu wa television fulani, ninafikiri ni Clouds TV.

"Ukaenda kwenye mji mwingine unakuta magunia ya bangi na dawa za kulevya, inaonyesha kuna kasoro kidogo kwa viongozi wanaoniwakilisha kule.

"Kuna OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya), kwa hiyo, IGP (Mkuu wa Polisi) ninataka OCD aondolewe Meru, DCO (Ofisa Usalama) Meru aondoke. Nani mwingine anayehusika na ulinzi pale? Maana yake hawakutimiza wajibu wao, waondolewe wote hasa Meru wale wanaojua kushikashika polisi, nani, nani... OCCID wote watoke na ikiwezekana wawe 'demoted' (washushwe vyeo), haiwezekani twende na utaratibu huo," aliagiza.

Kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Kamishna Kaji, Rais Magufuli alitangaza kumthibitisha kuwa kiongozi wa mamlaka hiyo mara moja na akaagiza kiapo chake kiandaliwe muda huo huo.

"Mimi ninataka mambo yaonekane, kwa sababu inasikitisha hadi dawa za kulevya mtu atoke Dar es Salaam akayaone wakati mkuu wa mkoa, wilaya, watendaji wengine wapo.

"Lazima ujue kuna 'syndicate' (makubaliano ya kushiriki) fulani. Baadhi ya wateuliwa, hawatimizi wajibu wao. Kwa hiyo, tunakuwa tunatengeneza taifa la mahali fulani la walevi wa dawa za kulevya," alisema.

Rais aliwataka wateule wake wapya kuhakikisha wanajituma kwenye maeneo yao na kutimiza wajibu wao.

"Niwapongeze wateule wangu ambao wengi wanatimiza majukumu yao, nawapongeza sana. Asilimia kubwa wanatimiza wajibu wao, ninajisikia raha kufanya kazi na wachapakazi.

"Ninamsikia (Martin) Shigela (Mkuu wa Mkoa wa Tanga) anazungumza hadi mtu fulani anatingishika, unajisikia raha. Taifa hili haliwezi kuwa la kuchezewa," alisema.

Rais Magufuli aliweka wazi kuwa kabla ya uteuzi, alilazimika kusoma vizuri jina la kila mteule, na kufuatilia aliyofanya, utendaji, wasifu wao na mahali walikopitia na kuridhika kuwa wataenda kufanya kazi waliyoteuliwa.

"Katibu Tawala Mkoa wa Simiyu, Mariam Mbaga, ninafahamu ulikuwa TAMISEMI tangu enzi za Alhaji Iyombe na amekutuma katika misheni mbalimbali za kuwatafuta watumishi hewa na walioghushi vyeti vyao mpaka wakakuchukia, ukatafutiwa mizengwe ya kila aina ya kusingiziwa kutokana na kazi nzuri uliyoifanya, yote nilikuwa ninafuatilia.

"Sasa, kutokana na ufuatiliaji wako, nikaona utatusaidia pale Simiyu kutokana na aliyekuwapo aliniomba ruhusa na nikamruhusu haraka sana. Kwa hiyo, kila mmoja ninafahamu. Ninawafahamu makatibu tawala niliowapandisha na kuwa wakuu wa wilaya.

# Bangi yaponza vigogo Polisi, Usalama Meru

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS John Magufuli ameagiza kuondolewa mamlaka na kushushwa vyeo Mkuu wa Polisi (OCD), Ofisa Usalama (DCO), Mkuu wa Upelelezi (OCCID) wa Wilaya ya Meru mkoani Arusha kutokana na kushindwa kudhibiti kilimo cha bangi.

Sambamba na hilo, amemthibitisha aliyekuwa Kaimu Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, James Kaji, kuwa Kamishna Jenerali wa mamlaka hiyo, baada kuridhishwa na utendaji kazi wake katika kupambana na dawa za kulevya, ikiwamo operesheni ya kukamata wanaolima bangi wilayani Meru.

Agizo hilo alilitoa jana wakati wa hafla ya kiapo cha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, wakiwamo wakuu wa mikoa ya Tabora na Kigoma na Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, iliyofanyika Ikulu jijini hapa.

Alisema ni vigumu kuwavumilia viongozi hao wa vyombo vya usalama kwa kamishna huyo kutoka Dodoma kwenda kukamata bangi wilayani Meru ilhali kuna viongozi kwenye wilaya hiyo.

"Ninawapongeza viongozi wengine ambao nimeshirikiana nanyi, vyombo vya ulinzi na usalama mmefanya kazi kubwa sana. Jana nilikuona wa dawa za kulevya ukienda kwenye milima kule na watu wa television fulani, ninafikiri ni Clouds TV.

"Ukaenda kwenye mji mwingine unakuta magunia ya bangi na dawa za kulevya, inaonyesha kuna kasoro kidogo kwa viongozi wanaoniwakilisha kule.

"Kuna OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya), kwa hiyo, IGP (Mkuu wa Polisi) ninataka OCD aondolewe Meru, DCO (Ofisa Usalama) Meru aondoke. Nani mwingine anayehusika na ulinzi pale? Maana yake hawakutimiza wajibu wao, waondolewe wote hasa Meru wale wanaojua kushikashika polisi, nani, nani... OCCID wote watoke na ikiwezekana wawe 'demoted' (washushwe vyeo), haiwezekani twende na utaratibu huo," aliagiza.

Kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Kamishna Kaji, Rais Magufuli alitangaza kumthibitisha kuwa kiongozi wa mamlaka hiyo mara moja na akaagiza kiapo chake kiandaliwe muda huo huo.

"Mimi ninataka mambo yaonekane, kwa sababu inasikitisha hadi dawa za kulevya mtu atoke Dar es Salaam akayaone wakati mkuu wa mkoa, wilaya, watendaji wengine wapo.

"Lazima ujue kuna 'syndicate' (makubaliano ya kushiriki) fulani. Baadhi ya wateuliwa, hawatimizi wajibu wao. Kwa hiyo, tunakuwa tunatengeneza taifa la mahali fulani la walevi wa dawa za kulevya," alisema.

Rais aliwataka wateule wake wapya kuhakikisha wanajituma kwenye maeneo yao na kutimiza wajibu wao.

"Niwapongeze wateule wangu ambao wengi wanatimiza majukumu yao, nawapongeza sana. Asilimia kubwa wanatimiza wajibu wao, ninajisikia raha kufanya kazi na wachapakazi.

"Ninamsikia (Martin) Shigela (Mkuu wa Mkoa wa Tanga) anazungumza hadi mtu fulani anatingishika, unajisikia raha. Taifa hili haliwezi kuwa la kuchezewa," alisema.

Rais Magufuli aliweka wazi kuwa kabla ya uteuzi, alilazimika kusoma vizuri jina la kila mteule, na kufuatilia aliyofanya, utendaji, wasifu wao na mahali walikopitia na kuridhika kuwa wataenda kufanya kazi waliyoteuliwa.

"Katibu Tawala Mkoa wa Simiyu, Mariam Mbaga, ninafahamu ulikuwa TAMISEMI tangu enzi za Alhaji Iyombe na amekutuma katika misheni mbalimbali za kuwatafuta watumishi hewa na walioghushi vyeti vyao mpaka wakakuchukia, ukatafutiwa mizengwe ya kila aina ya kusingiziwa kutokana na kazi nzuri uliyoifanya, yote nilikuwa ninafuatilia.

## HABARI KITAIFA

# Watiwa matatani tuhuma za kutorosha mabilioni ya NMB

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watu 32 wakiwamo wafanyakazi watano wa kampuni ya ulinzi ya Security Group of Africa (SGA) kwa madai ya kutorosha Sh. bilioni 2.8 mali ya benki ya NMB.

Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Juni 8, mwaka huu, baada ya walinzi hao kukabidhiwa fedha hizo ili kuzitoa tawi la NMB Mbezi Beach kwenda Makao Makuu, eneo la Posta Mpya.

Mambosasa alisema siku ya tukio, saa 9:00 alasiri, wafanyakazi hao wakiwa tawi la NMB Mbezi Beach, walikabidhiwa fedha hizo ili wazipeleke tawi la NMB House, 'Cash Centre'.

Alisema walinzi hao walitumia gari lenye namba za usajili T 853 DPX aina ya Mitsubish Canter kusafirisha fedha hizo, lakini badala ya kuzipeleka Posta walitoweka nazo.

"Siku hiyo ya tukio saa 12:00 jioni Jeshi la Polisi lilibaini kutekelezwa kwa gari hilo maeneo ya Mbagala Rangi Tatu jirani na Shule ya (Sekondari) Saint Mary's.

Kamanda Mambosasa alisema kikosi kazi cha kupambana na ujambazi kilianza ufuatiliaji na kilipofika eneo ambalo gari lilitelekezwa, walibaini walinzi hao walikula njama na kuziiba Sh. milioni 780.

"Fedha hizo waliiba kutoka kwenye sanduku moja la chuma kati ya masanduku waliyokabidhiwa. Masanduku matatu yaliyokutwa kwenye gari hilo yalipofunguliwa kulikutwa Sh. bilioni 1.3," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema ndani ya gari hilo walikuta silaha mbili aina ya Shotgun Pump Action yenye risasi 12 na Shorgun Protector yenye risasi tano pamoja na sare za kampuni yao ya ulinzi.

Alisema watuhumia hao walikamatwa mkoani Mbeya na Kigoma wakiwa tayari wameshanunua trekta power tiller aina ya TRA-Change Model 7C/15 lenye thamani ya Sh. milioni 20.

Pia alisema watuhumiwa hao walinunua pikipiki moja aina ya SUN LG, runinga moja ya kisasa 'flat screen' aina ya Sundar na vitu mbalimbali vya matumizi ya ndani kama kitanda, godoro, jiko la gesi na makochi.

Kamanda Mambosasa alisema mpaka sasa katika shauri hilo, kiasi kilichookolewa ni Sh. 1,497,680,000 mbali na thamani ya vitu vilivyonunuliwa kutoka sehemu ya fedha zilizoibwa.

"Jumla ya watuhumiwa 32 wamekamatwa na kuendelea kuhojiwa kuhusu ushiriki wao kuhusiana na tukio hili," alisema na kuongeza kuwa hakuna mhalifu ambaye atatenda kosa halafu akimbie nje ya mipaka ya Dar es Salaam akabaki salama.

Kamanda Mambosasa alisema tukio lililopita Jeshi la Polisi liliokoa Sh. bilioni 1.2 na wahusika wanaendelea na kesi ambayo ilihusisha benki ya NBC.

Alisema hakuna siri, walipewa hizo fedha na kamera zinaonyesha na Jeshi la Polisi limeahidi watahakikisha haki inatendeka na watakwenda kutoa ushahidi mahakamani.

"Tofauti ya kipindi hiki na vingine, fedha zilikuwa zikiondoka benki zilikuwa hazirudi zikienda huko hazirudi, kipindi hiki tutamfuatilia yoyote popote alipo tunamkamata na fedha zinarudi," alisema.

"Tumesema tutaanza ukamataji ni kweli, hizi fedha ni za watanzania kule tumehifadhi tu na za kwangu zipo kule maana yangu ni kwamba mshahara wangu unapitia NMB kwa hiyo pamoja na walioibiwa yupo Mtanzania anaitwa Mambosasa," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema kama watu wanaofanya kazi kwenye chumba cha ufuatiliaji kama walikula njama wana uwezo kuifanya isisome halafu baadaye wanategemea mgao kama ilivyofanyika kwenye tukio hilo kulikuwa na mgao karibu Sh. milioni 100 ulikuwa urudi kwa walioshiriki.

"Kifaa maalum cha kufuatilia mwenendo wa gari 'Car track' kinatusaidia sana, lakini wakitaka kujipanga isisomeke inawezekana, ila iwepo isiwepo tutaweka askari wetu kuhakikisha fedha zinatoka kwenye malindo na kwenda maeneo husika kwa usalama," alisema.




Katibu wa Masjid Al-waahab, Ahmed Haroun, akimtishwa ndoo ya majisafi na salama, Ester Joseph, mkazi wa Kata ya Nyandekwa, Halmashauri ya Mji wa Kahama, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa visima sita vilivyojengwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya International Istiqaama Muslim Community ya nchini Oman, katika kata hiyo, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Walimu matatani madai ya kuuza jina la mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

WALIMU watatu wa Shule ya Sekondari Kalenge, wilayani Biharamulo wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kagera kwa madai ya matumizi mabaya ya madaraka.

Walimu hao wanadaiwa kuuza jina la mwanafunzi wa kidato cha nne aliyekuwa mgonjwa kwa kumfukuza kwanza shule kwa madai ya utoro na baadaye jina lake kupewa mwanafunzi mwingine ambaye alifanya mtihani na kufaulu kwa daraja la pili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa, John Joseph, walimu hao walifanya udanganyifu wakati wa mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka 2019, huku wakijua mwanafunzi aliyefukuzwa alikuwa mgonjwa.

Aliwataja walimu hao kuwa ni Mkuu wa Shule hiyo, Boniphace Eliab, Makamu Mkuu wa Shule, Edwin Valentine na Mwalimu wa Taaluma, Grevas Richard.

"Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba walimu hao walimfukuza shule mwanafunzi mmoja (jina limehifadhiwa) kwa kisingizio cha kuwa alikuwa mgonjwa na kisha wakati wa mitihani wa kwa njia za rushwa waliitumia namba yake kumpa mwanafunzi mwingine ambaye aliufanya mtihani huo," alisema na kuongeza:

"Uchunguzi wetu umebaini pia baada ya matokeo kutoka, jina la mwanafunzi aliyekuwa amefukuzwa lilioneka kuwa amefaulu kwa kupata daraja la pili, huku inafahamika kuwa mwanafunzi halisi mwenye jina hilo alishafukuzwa na hakufanya mtihani."

Kwa mujibu wa Joseph, hali hiyo ilimfanya mzazi wa mwanafunzi aliyefukuzwa kushikwa na mshangao na kuamua kutoa taarifa TAKUKURU.

Alisema uchunguzi ulibaini kuwa wakati mwanafunzi huyo mgonjwa wa macho ametaarifiwa juu ya kufukuzwa, uongozi wa shule kwa njia za rushwa ulimwingiza mwanafunzi mwingine (jina limehifadhiwa), ambaye alifanya mtihani wa kuhitimu kwa jina na namba ya mwanafunzi aliyedaiwa kufukuzwa. "Matokeo yalipotoka yalionyesha jina na namba ya mwanafunzi aliyedaiwa kufukuzwa kwamba amefaulu kwa daraja la pili, huku mwanafunzi halisi akiwa hakufanya mtihani wowote," alisema.

"Kutokana na taarifa hizo TAKUKURU iliamua kuwashikilia walimu wote kwa mahojiano zaidi," alisema.

# Kitendawili mgombea CUF sasa kuteguliwa Julai 27

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema kuwa majina ya wagombea urais walioomba ridhaa ya kupitishwa na chama kupeperusha bendera ya chama hicho yatajulikana Julai 27.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai, wagombea hao watajulikana kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa wa chama hicho.

"Mchakato ndani ya chama unaendelea, utahitimishwa Julai 27, kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa ambako mgombea urais Bara na Zanzibar watapatikani," alifafanua Kilaghai.

Wakati CUF wanatarajia kutangaza wagombea wake, tayari baadhi ya vyama ikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na ACT –Wazalendo vimeanza mchakato wa kuwatafuta wapeperusha bendera katika nafasi hiyo.

CCM Bara tayari aliyerudisha fomu ni mtiania pekee, Rais John Magufuli wakati upande wa chama hicho Zanzibar tayari majina ya watiania watano wa nafasi hiyo wameshapatikana na kupelekwa Dodoma kwa ajili ya mchujo mwingine wa kutafuta jina la mgombea mmoja.

CHADEMA, ACT-Wazalendo na NCCR-Mageuzi bado vipo katika hatua ya watiania kuchukua fomu kwa ajili ya kuomba kuteuliwa.

Kwa upande wa NRA, TLP na UDP, vimetangaza kutosimamisha mgombea katika nafasi ya urais badala yake vimesema vitampigia kampeni Rais Magufuli endapo atapitishwa na chama chake kuwania nafasi hiyo.

Kwa upande wa CHADEMA, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, amechukua fomu ya kuomba kuteuliwa kupeperusha bendera ya chama hicho kwa upande wa Tanzania Bara, wakati kwa upande wa Zanzibar aliyechukua fomu kuwania nafasi hiyo ni Hashimu Juma Issa.

RIPOTI MAALUM

# Jumuiya Burunge hifadhi inayosimama kwa mtindo wa serikali, bajeti mabilioni

## Iko na vijiji 10, kimoja kina Sh. mil. 500 ▌Vina shule, zahanati, nyumba za walimu...

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa BABATI**



Diwani wa Kata ya Mwada, Gerald Chembe, akionyesha jengo la bweni la wanafunzi katika Shule ya Sekondari Mbungwe, wilayani Babati, mkoani Manyara. **PICHA: SALOME KITOMARI**

NI nadra kwa kijiji kuwa na uwezo wa kutimiza huduma za kijamii kwa kutumia mapato yake, huku kikiwa na akiba Sh. milioni 500 benki zinazosubiri kupangiwa matumizi ya maendeleo.

Lakini, unapotembelea vijiji 10 vya Kata za Nkaiti, Mwada na Magara katika Tarafa ya Mbugwe wilayani Babati mkoani Manyara, utayaona makubwa ya huduma za kijamii kama majengo ya shule, nyumba za walimu, zahanati, vituo vya afya na ofisi za vijiji za kisasa, ni vigumu kupata mfano wake katika vijiji vingine.

Katika vijiji hivyo, pia kuna ushuhuda wa ujenzi wa majengo ya shule mpya na huduma nyinginezo za kijamii. Siri ya mafanikio hayo ni nini? Fedha zinazotokana na utalii, kwenye Jumuiya ya Hifadhi za Jamii (Burunge Wildlife Management Area -WMA).

Ni kwamba, kila kijiji kinanufaika na mgao wa mamilioni ya shilingi kwa ajili ya kutekeleza maendeleo yao kwa mujibu wa vipaumbele walivyojiwekea.

Nipashe ilifanya ziara ya kuchunguza kupata undani wa uhalisia huo kwa uwezeshaji wa Shirika la Internews chini ya Mtandao wa Waandishi wa Habari Duniani (Earth Journalist Network).

Sura pana ya manufaa hayo, imebainika kuwezeshwa kujiendeleza kielimu kwa ngazi mbalimbali kwa watoto kutoka familia zisizojiweza kiuchumi. Hapo kuna maana ya ngazi kama vyuo vya ufundi hadi kileleni vyuo vikuu.

Kimsingi, kitaifa kuna jumla ya jumuiya 38. Kati yake, 16 ndiyo zimesajiliwa, ambazo mbali na Burunge, nyinginezo ni Iyumbu, Ipole, Ikona, Makao, Enduiment, Wami Mbiki, Ukutu, Tunduru, Mbaragandu, Liwale, Ngarambe Tapika na Idodi Pagawa.

Burunge inashika nafasi ya pili kimapato ikikusanya Sh. bilioni 2.3, ikitanguliwa na Serengeti inayokusanya Sh. bilioni 2.7 kwa mwaka.

Katibu wa Jumuiya ya Burunge, Benson Maise, anafafanua utaratibu wa mgao wa mapato, kwamba nusu hubaki kwenye jumuiya kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na kinachobaki hupelekwa kwenye vijiji 10 vilivyo katika ubia na hifadhi hiyo.

Tafsiri ya mafanikio yaliyoko vijijini, ni kwamba vinamiliki hoteli za kitalii zenye wateja mamia ya wageni hifadhini, ambazo manufaa yake yanaenda moja kwa moja kijijini.

Mfano hai wa mafanikio hayo, unaonekana katika Kijiji cha Sangaiwe chenye akiba ya Sh. milioni 500 benki kwa ajili ya matumizi kama vile ujenzi wa shule, zahanati na miradi ya barabara na maji.

Katibu huyo anafafanua vigezo vya mgao, inapotokea kijiji kinashindwa kutunza eneo la hifadhi, kinanyimwa fedha hizo hadi kitakaporekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mafanikio yaliyopo hadi sasa, wakazi wa vijiji vyote 10 hawachangishwi fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyowahi kujitokeza huko nyuma katika hatua za kujipanga walipochangisha Sh. 70,000 kwa kila kaya.

Maise anasema, kwa sasa akiba ipo na kinachofanyika ni fedha zinatumika kwa mujibu wa bajeti na mipango iliyopitishwa na mkutano mkuu wa kijiji.

**DIWANI ANENA**

Diwani wa Mwada, Gerald Chembe, ambako ndiyo makao makuu ya WMA, anasema vyombo vya usafiri vilivyopo, pia vinatumika kuwapeleka wanavijiji katika mahitaji kama hospitali, shughuli za kiuchumi na kijamii.

Chembe ambaye yumo katika waanzilishi wa WMA hiyo, anasema walianza na wazo la uchumi wa uhifadhi na wakalitekeleza kwa kutoa elimu kwa kushirikiana na Africa Wildlife Foundation, na wakapata mwitikio wa wananchi ambao waliridhia sehemu ya ardhi yao kuingizwa kwenye jumuiya.

"Tulianza kama hifadhi ya jamii, nami nilikuwa katibu wa kamati ya usimamizi wa mazingira. Tulipeleka baadhi ya wananchi kusoma, wakati huo tulikuwa tunatembea porini kwa miguu na baiskeli na bado baadhi walikuwa hawaoni umuhimu kwa kuwa waliendelea kukata miti na kulisha mifugo.

"Kuna vitu tuliruhusu kama wazee anapotaka miti kwa ajili ya shughuli za kienyeji na hupewa kibali na kusindikizwa na askari, na waliruhusu kunapokuwa na shida ya kuni kwa ajili ya shughuli za jamii, kijiji kinaandika barua anaruhusiwa kuokota kuni kavu," anasimulia. Diwani anakiri manufaa waliyopata, mbali na kuni, wakazi walipata dawa na mahitaji mengineyo katika kata hiyo yenye vijiji vitatu na baada ya kupatikana wawekezaji kwenye WMA, biashara ya utalii ilianza mara moja na mapato yakaanza kuonekana, huku kukiwapo manufaa ya moja kwa moja vijijini.

"Mgao wa sasa ni zaidi ya Sh. milioni 100 kwa kila kijiji. Tunakaa kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) na kuainisha vipaumbele vya kila kijiji na tunakwenda kwenye mkutano wa kijiji kuwaeleza na baada ya kupitishwa, fedha hutolewa kwa usimamizi wa halmashauri," anafafanua.

Anaeleza utaratibu uliopo, kila mamlaka iliyoidhinishiwa matumizi, fedha huwekwa kwenye akaunti yake, mathalani akaunti za shule zinazosimamiwa na bodi ya shule kutekeleza mradi, chini ya kamati ya ujenzi.

"Kutokana na fedha hizi katika Shule ya Sekondari ya Mbugwe, tumejenga matundu 36 ya vyoo, madarasa, hosteli na miundombinu ya shule. WMA ilitoa Sh. milioni 19 za ukarabati wa madarasa matatu na madawati 100. Kwa ujumla, miradi ya shule hiyo ni zaidi ya Sh. milioni 300. Kwa sasa tunajenga bwalo litakalotumiwa na wanafunzi 1,000," anasema.

Chembe anafafanua wamejenga vyoo vya kisasa vinavyokidhi mahitaji ya makundi yote shuleni, wakiwamo watu wenye ulemavu.

"WMA imesaidia kusukuma maendeleo kwa haraka zaidi kuliko kata zilizozunguka Halmashauri ya Babati. Nguvu ya halmashauri kugawa fedha kwa kata 25 ni ngumu sana. Ubunifu huu umevifanya vijiji vyetu kufanya maendeleo kwa fedha zao.

"Uhifadhi umetuwezesha wananchi kujua kukata miti, kuua mnyama ni vibaya na ndiyo maana wanyama wapo. Ukitembelea kata yangu, tumefanya miradi mikubwa, utadhani fedha zimetoka Serikali Kuu, kumbe ni faida ya uhifadhi," anasema.

Anaendelea kuwa WMA ilikofikia sasa, ni hatua ya kuwekeza kwenye miradi mikubwa, kama ujenzi wa shule, huku ikimiliki magari na trekta, huku halmashauri nayo ikinufaika kwa mgao wa zaidi ya Sh. milioni 200 kwa mwaka.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Lawrence Mukebe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwada, anasema fedha walizopata tangu mwaka 2012, zimewazesha kujenga ofisi kubwa ya kijiji, akijigamba ikiwa na ubora wa kipekee katika Halmashauri ya Babati yenye huduma kama ukumbi, stoo, ofisi ya mtendaji wa kijiji, masjala na ofisi za wataalamu.

Anataja miradi ya maendeleo na kiasi cha fedha kilichotolewa katika mabano kwa kila mradi ni: Madarasa matatu ya Shule ya Msingi Mbugwe (Sh. milioni 44.3); choo (Sh. milioni 26.7); mfumo wa maji (Sh. milioni 3.5); na ukarabati wa zahanati ya kijiji (Sh. milioni 33).

Mingine ni: Kukarabati maabara (Sh. milioni 3.7); choo cha shule ya sekondari (Sh. milioni 18); hosteli (Sh. milioni 16); jengo la utawala (Sh. milioni tisa); umeme kwenye madarasa (Sh. milioni 9.9); na kukamilisha ujenzi wa nyumba mbili za walimu, ambazo wanakijiji walitakiwa kuchangia maji katika ujenzi.

Anadokeza mipango inayoendelea mwaka huu ni: Kujenga madarasa mawili; ofisi ya walimu; umeme ofisi ya kijiji; ujenzi wa nyumba ya matabibu wawili na huduma ya umeme.

"Serikali ya kijiji tunashiriki kulinda eneo ulilolitoa na kuunda WMA. Tunatunza, tunakamata mifugo na wanatozwa faini kulingana na taratibu tulizojiwekea. Hatufanyi mradi wowote bila kushirikisha wananchi, ni lazima wapitishe kwenye mkutano mkuu wa kijiji," anasema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mbugwe, Justine Ndikile, anaunga mkono kwamba jumuiya imewezesha shule kuwa na miundombinu bora, yakiwamo madarasa ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

"Tayari kijiji kimepitisha miradi ya kipaumbele kwa mwaka huu kuwa ni kujenga ghala la mazao na kuingiza umeme kwenye madarasa yote. Walimu wana makazi, zote hizi ni kutokana na nguvu za uhifadhi zinazofanywa na jamii," anasifu.

*ITAENDELEA KESHO

# Kampuni hewa kufutwa

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeagiza kufutiwa usajili kampuni zote zilizosajiliwa kwa ujanja ujanja ambazo zimekuwa hazihusishi tarifa na wala hazijulikani zilipo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, alisema hayo jana wakati akizungumza na viongozi na wafanyakazi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), jijini Dar es Salaam.

Shemdoe alisema kampuni hizo zimesajiliwa kwa ujanja ujanja na kutelekezwa na wahusika, hivyo kuna umuhimu wa kuandaa utaratibu wa kuhakikisha zote zinafutiwa usajili.

"Kama kuna ugumu wa kuzifuta kutokana na kanuni au sheria tuandikieni wizara ili Bunge lijalo tuwasilishe muswada tufanye marekebisho ya sheria tuzifute tubaki na kampuni halali zinazofanya kazi," alisema Shemdoe.

Alisema anajua kwamba BRELA inadai fedha nyingi kwa kampuni hizo, lakini ikijaribu kuzitafuta hazizipati kwa sababu haziko popote.

Prof. Shemdoe pia aliwataka wafanyakazi wa BRELA kufanyakazi kwa uadilifu kwa kuwa taasisi hiyo inavishawishi vya rushwa, huku akisisitiza kwa mtumishi yeyote atakayehusika na rushwa afukuzwe.

"Kama kuna mtu hawajibiki sehemu yake ashughulikiwe maana tumeingia kwenye uchumi wakati sasa tunapaswa kudhihirisha hili kwa kuhakikisha kila mtu anawajibika sehemu yake," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alisema wamekuwa na mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (ORS) ambao unalalamikiwa sana na wateja kutokana na kutokuwa rafiki kwenye matumizi yake.

Alisema wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa taasisi hiyo wanausuka upya mfumo huo ili kuondoa kero zilizokuwa zinajitokeza mara kwa mara.

Nyaisa alisema kumekuwa na nyaraka ambazo zinahitaji kuandaliwa upya kwa kuwa zilizopo muda wake unakaribia kwisha na kumekuwa na nyaraka muhimu za kiutendaji ambazo hazikuwapo kabisa.

"Hali hii ilisababisha hata watoa maamuzi kufanya baadhi ya maamuzi kwa utashi wao bila kufuata sheria, kanuni na taratibu za kiutendaji," alisema.



Meneja wa Maduka ya Rejareja wa Vodacom Tanzania PLC, Vanessa Mlawi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, waliotembelea banda la Vodacom kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu punguzo kubwa la bei kwa simu za Smart Kitochi, na bidhaa mbalimbali zinazopatikana bandani hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yapongezwa kuingia uchumi wa kati

**Na Romana Mallya**

BANCABC imeipongeza serikali kwa kuwezesha nchi kuingia kwenye uchumi wa kati na kuahidi kuendelea kutoa huduma za mikopo zenye riba nafuu kwa wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa ili waweze kukuza biashara zao.

Mkuu wa Kitengo cha Hazina ndani ya benki hiyo, Barton Mwasamengo, aliyasema hayo jana katika maonyesho ya 44 ya biashara yanayoendelea viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam.

Mwasamengo alisema benki hiyo inaunga mkono juhudi za serikali za kuipeleka nchi kwenye uchumi wa kati kwa kuwawezesha wafanyabiashara wa aina zote kupata fursa ya mikopo ya riba nafuu.

Pia alisema kutokana na changamoto ya ugonjwa wa corona ambayo imekumba nchi mbalimbali duniani, benki yake katika kumjali mteja wanaangalia namna ya kumpa unafuu wa kurejesha mkopo.

"Kwa wateja waliokopa na ambao hawajakopa tumefungua milango hasa kutokana na janga hili la corona tumekuwa tukiwapa unafuu wa riba wa namna ya kurejesha mikopo yao," alisema.

Alisema wanatoa mikopo ya watu binafsi ili kuendeleza shughuli ndogo ndogo kama za mama lishe.

Alisema katika maonyesho hayo wamelenga kuonyesha bidhaa za mikopo wanayoitoa, kufungua akaunti ambayo kila mwezi inapata riba kwa mwenye salio kuanzia Sh. 10,000, haina makato ya kila mwezi na haina kima cha chini cha kuendesha akaunti.

Pia alisema wanafanya huduma za kibenki kidigitali ambazo mtu ahitaji kuwa na akaunti na anaweza kufanya ununuzi kupitia mtandao.

Mwisho

## DIT yazindua mashine ya wagonjwa kupumua

**Na Gwamaka Alipipi**

TAASISI ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), imebuni mashine ya kumsaidia mgonjwa aliyeshindwa kupumua (ventilator), wakati huu wa uwapo wa ugonjwa wa virusi vya corona.

Mashine hiyo imebuniwa na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa chuo hicho kwenye fani ya stashahada ya uhandisi vifaa tiba, kwamba wameitengeneza kwa muda wa miezi miwili.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, mmoja wa wanafunzi hao, Inocent Dogras, alisema walilazimika kutengeneza kifaa hicho baada ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa corona na kusababisha vifo vya watu wengi duniani.

"Baada ya kusikia kuwa Ventilator ni gharama kubwa kuinunua na wagonjwa wengi walikuwa wanafariki kwa kukosa kifaa hicho, hivyo tulilazimika kukitengeneza ili kuwasaidia wagonjwa hususani wanaoishi vijijini ambao hawana uwezo wa kumudu huduma za afya," alisema Dogras.

Aliongeza kuwa DIT wamewapa msaada wa vifaa kwa ajili ya kutengeneza na kwamba kwa sasa hivi wameshakamilisha na kipo tayari kwa matumizi.

Mwanafunzi mwingine aliyeshiriki katika kutengeneza kifaa hicho, Aiche Rodgers, alisema kifaa hicho kazi yake ni kumsaidia mgonjwa kuingiza na kutoa hewa nje.

"Mgonjwa anapozidiwa kupumua tunamvalisha face mask ambayo kwa asilimia 80 hadi 90 inamsaidia kuingiza na kutoa hewa nje, alafu mashine hii (Ventilator) ndiyo itakayomsaidia kupumua vizuri kwa muda wote hadi atakapopona," alisema Rodgers. Ofisa uhusiano wa DIT, Amani Kakana, alisema uongozi wa chuo umewapa elimu ya ubunifu wanafunzi hao ambao umewawezesha kubuni kifaa hicho, kwamba lengo kuu la DIT ni kuhakikisha changamoto zilizopo katika jamii zinatatuliwa.

Kakana alisema baada ya kuingia kwa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona ndipo lilipobuniwa wazo la kutengeneza mashine hiyo, baada ya kusikia kwamba kuna upungufu.

Alisema DIT iliwawezesha vifaa wanafunzi hao pamoja na fedha ili waweze kukamilisha ubunifu wa kifaa hicho ambacho hadi sasa kimeshakamilika kwa asilimia mia.

Kakana alisema: "Huwa tunatenga fedha kwa ajili ya miradi inayotatua changamoto katika jamii, hivyo kwa wahaa wanafunzi tuliwasilikiza mahitaji yao kasha sisi tukaenda kununua vifaa wanavyovihitaji."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uvumilivu utawale uteuzi wagombea kwenye vyama

MCHAKATO wa Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa Oktoba, mwaka huu umeanza rasmi.

Vyama vimesharuhusu wagombea watiania ya urais kuanza kutangaza nia pamoja na uchukuaji wa fomu ndani ya vyama kuomba uteuzi ili kupeperusha bendera za vyama hivyo katika uchaguzi huo.

Baada ya utangazaji wa nia na uchukuaji wa fomu, hatua itakayofuata ni vyama vya siasa kuwashindanisha watiania kisha kuteua mmoja.

Kwa mfano, katika Chama Cha Mapinduzi (CCM) mchakato wa kuomba uteuzi kwa ajili ya urais wa Zanzibar umeshafungwa, baada ya watia nia zaidi ya 30 kuomba kisha kuchujwa na kubakizwa majina matano. Kadhalika, pazia la kuomba uteuzi wa kugombea urais limeshafungwa, baada ya kujitokeza mtiania mmoja, Rais John Magufuli.

Tunafahamu kuwa mchakato wa uteuzi ndani ya vyama kuwa una changamoto nyingi na ngumu, kwa kuwa kila atakayechukua fomu kuomba kuteuliwa na chama chake, atakuwa amejipima na kuona kuwa anatosha kuteuliwa.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeshafunga pazia la watiania ya urais baada ya kujitokeza makada 11 kwa urais wa Jamhuri ya Muungano na mmoja kwa Zanzibar, huku mmoja, Tundu Lissu, akichukua fomu.

Kwa upande wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amechukua fomu ya kuomba uteuzi kugombea urais wa Zanzibar wakati kwa Jamhuri ya Muungano watiania katika vyama vingine bila shaka wataendelea kujitokeza kwa mujibu wa ratiba za vyama vyao.

Tunatarajia kuanza kuona mchakato huo ukiingia ngazi ya udiwani na ubunge ndani ya vyama kabla ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza ratiba rasmi ya uchaguzi mkuu.

Kwa kuwa mchakato huo wa ushindani ndani ya vyama una changamoto nyingi na kubwa, tunawashauri watia nia wote kuwa wastaarabu kwa kufanya kampeni zao za ndani kwa njia ya kistaarabu.

Tunatoa ushauri huo kwa kuwa uzoefu wetu unaonyesha katika chaguzi zilizopita tulishuhudia watiania wakikosa ustaarabu badala yake kutumia njia za kuchafuana, kutukanana, , fitina na kupikiana majungu.

Aidha, tuliwahi kushuhudia watiania wa chama kimoja wakisingiziana, ikiwamo kutuhumiana kwa vitendo vya rushwa. Lengo la haya yote ni mbinu za kuteuliwa.

Rai yetu kwa watiania wote ni kujiepusha na vitendo vyote ambavyo ni ukiukaji wa maadili, badala yake wajielekeze katika kuwashawishi kwa hoja wapigakura ambao ndio watakaoamua hatima yao kwa njia ya kura.

Watiania wenye sifa za uchapakazi, uadilifu, ubunifu, tabia njema, uzalendo na wapenda watu hawana sababu ya kutumia njia za mkato, zikiwamo za kukiuka maadili kwa kuwa wana nafasi kubwa ya kupitishwa na vyama vyao.

Hata hivyo, changamoto kubwa ambayo imekuwapo siku zote ni suala la rushwa, ambayo imekuwa ikitolewa kwa wajumbe wa vikao vya kupiga kura za kuwapitisha wagombea kupitia kwa wapambe na mawakala wa wagombea.

Kwa bahati nzuri Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) umeshaeleza wasi kuwa haitakuwa na suluhu na mtu yeyote ambaye atabainika kuhusika katika rushwa wakati wote wa mchakato wa uchaguzi wa mwaka huu.


Jambo la kutia moyo ni kuwa TAKUKURU imeshaonyesha kwa vitendo kuwa haitanii kwa hili, kutokana na kuanza kuwakamata watuhumiwa mbalimbali bila kujali nafasi zao wala vyama wanavyotoka.

Tunasisitiza kuwaomba watiania wote katika kipindi hiki cha mchakato wa uteuzi ndani ya vyama kuwa wavumilivu; kwa maana ya kushindanisha hoja na kuvumiliana ili kuthibitisha kuwa jamii ya Watanzania ni ya watu wastaarabu.

Tunatarajia kuwaona watakaoshindwa wakikubali kushindwa na kuwaunga mkono watakaoteuliwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Habari njema Tehama isiishie shule za mijini

Na Sabato Kasika

ILI kuwawezesha wanafunzi kufahamu matumizi ya taarifa mbalimbali, kumudu vyombo vya mawasiliano na kujifunza kupitia maktaba, serikali ilianzisha somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) shuleni.

Kozi hiyo ilianza kufundishwa mwaka 2005 katika mtalaa mpya wa Elimu ya Msingi.

Hii inatokana na ukweli kwamba katika dunia ya sasa ya utandawazi, matumizi ya Tehama hususani kompyuta yamechangia kuendeleza na kusambaza matumizi ya sayansi na teknolojia.

Kwa hapa Tanzania, Kiswahili kinatumika kama lugha rasmi ya kufundishia somo hilo, shule za msingi kama nyenzo ya kuwasilisha elimu ya sayansi na teknolojia ya kisasa kwa wanafunzi.

Pamoja na juhudi hizo za kuanzisha kwa somo hilo, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine, zinazoweza kukwamisha ufundishaji na ujifunzaji wa Tehama.

Baadhi ya changamoto hizo ambazo zimewahi kutajwa na wizara husika ni uhaba wa walimu, ukosefu wa umeme hususani maeneo ya vijijini na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Kwa upande wa serikali, inajitahidi kutatua changamoto ya nishati kwa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), ili kuhakikisha somo hilo linafundishwa katika ngazi zote linapohitajika.

Lengo la kufanya hivyo, ni kuwaandaa walimu watakaofundisha somo hilo shuleni, huku ikishirikiana na kampuni ya Microsoft kwa ajili ya kupata vifaa hasa kompyuta.

Huo ni mpango wa muda mrefu wa serikali wa kuimarisha matumizi ya somo hilo katika ufundishaji shuleni, lakini kwa sasa linafundishwa kwa baadhi ya shule na hasa za mijini ambazo zina mazingira rafiki ikiwamo umeme.

Kwa sehemu hizo ni wazi kwamba kuna umuhimu wa kuwaandaa walimu na pia kuhakikisha shule zote zinakuwa na umeme ili iwe rahisi kwa walimu kufundisha na pia iwe rahisi kwa wanafunzi kuelewa.

Ukisoma kitabu cha Tehama darasa la saba, kuna mada kama vile mtandao wa ndani wa kompyuta, mtandao wa intaneti, kutumia tovuti, maana ya baruapepe, hayo yote walimu na wanafunzi wanatakiwa kuyaelewa.

Sidhani kwamba walimu na wanafunzi wa shule za vijijini wanaweza kuyaelewa, hivyo kuna haja ya kuhakikisha shule zote zinakuwa na walimu wanaojua matumizi ya Tehama ili iwe rahisi kufundisha somo hilo.

Walimu itawawia rahisi kufundisha iwapo pia shule zitakuwa na umeme kwa ajili ya kompyuta, hivyo ni vyema kasi ya kusambaza umeme ya REA ikaongezwa ili shule zote ziwe na nishati ya umeme.

Shule za vijijini zisionekane kama zinabaguliwa kwenye somo la Tehama, kwa sababu ya kukosa nishati ya umeme, kwani huko nako kuna wataalam wa baadaye ambao wanahitaji kusoma somo hilo.

Hayo yakifanyika, wanafunzi wa shule za vijijini hawatakuwa nyuma kwenye somo hilo, hivyo umeme usambae kote, wizara husika iandae mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wa vijijini ambao watafundisha Tehema.

Kama umeme unaweza kuchukua muda mrefu, basi uangaliwe uwezekano wa kuhakikisha shule zote zinakuwa na umeme jua ili kurahisisha ufundishaji wa somo hilo.

Siyo vibaya kushirikisha wadau wote wa elimu kwa ajili ya kufanikisha somo hilo kwa shule zote nchini, kwani wanaweza kusaidia upatikanaji wa kompyuta mpakato, sola na huduma nyingine muhimu.

Wakati hilo likifanyika, wizara nayo iwajengee walimu uwezo katika somo hilo, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano duniani, ambayo kimsingi huathiri nyanja mbalimbali za maisha.

Hayo yakifanyika, kutakuwa na mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo nchini, bila kujali kwamba ni za vijijini au mijini, kwani kila moja itakuwa na mahitaji yote muhimu.

Pamoja na hayo, ninaamini kwamba kuna manufaa mengi katika ufundishaji wa somo hilo kwa lugha ya Kiswahili, kwani kunasaidia kujenga saikolojia ya kujiamini na kujithamini miongoni mwa wanafunzi.

Vilevile kutumia lugha hiyo ni hatua muhimu ya kukabiliana na mahitaji mapya katika medani za sayansi na teknolojia, tofauti na sura yake ya kuwa lugha ya kwenye majukwaa ya kisiasa, nyumbani na maeneo mengine.

# Taasisi za kisheria zaonywa kupiga kampeni za kisiasa

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

TAASISI zinazotoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa msaada wa kisheria zimeonywa kujiingiza katika masuala ya kisiasa ikiwamo kuwapigia kampeni wagombea katika uchaguzi mkuu ujao.

Kauli hiyo imetolewa jana mkoani Tabora na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria na Katiba, Amon Anastizi Mpanju, wakati akizindua Kamati ya Uratibu wa Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa ngazi ya mkoa.

Alisema watoa huduma wa msaada wa kisheria na wasaidizi wa msaada wa kisheria waliosajiliwa hawapaswi kutumia mlango wa huduma ya msaada wa kisheria kufanya kampeni za kisiasa.

"Tupo katika majira ambayo tunaelekea katika kampeni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani...Taasisi zilizosajiliwa kama watoa huduma wa msaada wa kisheria zile 11 na wasaidizi wa msaada wa kisheria wasitumie mlango wa huduma za kisheria kufanya siasa," alisema.

Aliwataka viongozi wa kamati hiyo ya Mkoa wa Tabora kuzichukulia hatua taasisi zote zitakazobainika kufanya kampeni ya kisasa kwa kuwa zitakuwa zinakiuka masharti na taratibu za usajili wao.

Aliwataka wajumbe wa kamati hiyo ya mkoa kuhakikisha kuwa hakuna masuala ya ushoga na usagaji yatakayoruhusiwa kuingia mkoani humo kwa sababu ni kinyume cha utamaduni wa kitanzania na sheria za nchi.

"Nawaombeni msiruhusu masuala ya ushoga na usagaji yaingie mkoani Tabora kwa sababu yanakwenda kinyume na sheria zetu na utamaduni wa Mtanzania," alisisitiza.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Mangwi, Twahiru Ndombogo (katikati), akipokea msaada wa vifaa vya ofisi na tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 17 kutoka kwa Meneja Maendeleo ya Uchumi wa Jamii wa kampuni ya Songas, Nicodemus Chipakapaka, kwa ajili ya zahanati ya kijiji hicho wilayani Kibiti mkoani Pwani, jana. Kushoto (mwenye miwani) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mohammed Mavura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 15 wajitokeza ubunge kupitia CHADEMA Dodoma

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WATIA nia 15, wa nafasi ya ubunge, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wamejitokeza kuchukua fomu ya kuwania nafasi hiyo katika majimbo 10, ya mkoa wa Dodoma.

Jimbo la Dodoma mjini ambalo lilikuwa likiongozwa na Naibu Waziri Ofisi wa Waziri mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Antony Mavunde, linaongoza kwa kuwa na watiania sita, waliochukua fomu hadi jana asubuhi.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari na Uhusiano wa CHADEMA kanda ya Kati, Juma Omary, alisema kuwa hadi kufikia jana asubuhi watia nia 15, walikuwa wamechukua fomu katika majimbo yote 10, ya mkoa wa Dodoma.

Alisema kuwa, katika jimbo la Dodoma mjini, tayari watia nia sita wamechukua fomu za kuwania nafasi hiyo ya Ubunge.

"Katika majimbo mengine kama Bahi amechukua mmoja, Kondoa mjini wawili, Kondoa Vjijini wawili, Mpwapwa wawili, Chilonwa mmoja, Kibakwe mmoja, Kongwa wawili pamoja na jimbo la Mtera wawili," alisema.

Aliyataja majina ya watia nia katika jimbo la Dodoma Mjini waliochukua fomu mpaka sasa kuwa ni Tuli Kiwanga, Aisha Madongo, Amoni Muhembo, Saidi Kitegile na kudai kuwa wengine bado wanaendelea kuthibitishwa kutokana na kuchukua fomu kwa njia ya mtandao.

Kadhalika alisema, watiania wengine waliochukua fomu ni Hadija Maula na Monica Azaria, (Jimbo la Mtera) Amina Idd na Idd Kizota (Kondoa Mjini),Kunti Majala na Rongo Bura(Chemba), Ramadhani Abdi na Monica Safari (Kondoa Vijijini).

Aliongeza kuwa, watia nia wengine ni Mussa Makuo, (Mpwapwa), Silvester Luzua (Kibakwe) pamoja na Neema Chiuyo Jimbo la Kongwa.

Pia Omary alisema changamoto ambayo wamekuwa wakikutanayo hivi sasa watia nia wao ni kukamatwa na polisi baada ya kuchukua fomu.

"Katika maeneo kama Morogoro, Singida watia nia wetu wamekamatwa nakuhojiwa na Jeshi la Polisi hali ambayo inawatishia wengine wasijiokeze, hivyo tunaliomba Jeshi la Polisi kuwaacha watia nia wetu watekeleze haki yao ya kikatiba," alisema Omary

Vile vile alisema kuwa watiania katika nafasi ya udiwani ndani ya chama hicho wataanza kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo kuanzia Julai 11 hadi 17, mwaka huu katika maeneo mbalimbali ya nchi.

## TASAF yalipa kaya maskini kielektroniki

**Na Sara Magesa, GEITA**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani Nyang'wale, mkoani Geita, umeanza kulipa fedha kwa njia ya kielektroniki, ili kupunguza gharama na kuondoa udanganyifu kutoka kwa watendaji wasio waaminifu.

Fedha hizo hutolewa chini ya mpango wa kunusuru kaya maskini, awali walilipwa kupitia dirishani na kusababisha kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya watendaji kulipa fedha pungufu pale walipoona mhusika hanauwezo wa kutambua.

Hayo yamesemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TASAF, Zuhura Mdungi, wakati akitoa mafunzo ya namna ya kufanya uhakiki wa kutambua kaya maskini katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya mfuko huo.

Akizungumzia mzunguko wa tatu wa TASAF, alisema lengo la uhakiki ni ili kubaki na walengwa wenye vigezo na kuwaondoa walengwa wasio na sifa ya kubaki kwenye mpango wa TASAF.

Alisema TASAF kipindi cha pili ilifikia asilimia 70 za vijiji vyenye walengwa kote nchini, huku asilimia 30 ikibaki kutokana na ukosefu wa fedha, na kwamba awamu ya tatu itawatambua walengwa wote kwa asilimia 100.

Aidha, alisema uhakiki huo utawaondoa walengwa ambao tayari wamejikwamua kiuchumi baada ya kuwezeshwa kwenye awamu ya pili.

Kipindi cha pili cha awamu ya tatu TASAF inategemea kuzifikia kaya milioni 1.4 zenye watu milioni saba nchini, na kwamba mkazo umewekwa katika kuwezesha kaya zitakazoandikishwa kwenye kufanya kazi ili kuongeza kipato.

Naye, Mratibu wa TASAF Wilaya ya Nyang'wale, Nashon Magumba, alisema katika halmashauri hiyo walengwa ni 3,089, na kwamba utekelezaji wa awamu ya pili umewakwamua walengwa kiuchumi kwa kuanzisha miradi iliyowatoa kwenye lindi la umaskini.

**Alisema TASAF kipindi cha pili ilifikia asilimia 70 za vijiji vyenye walengwa kote nchini, huku asilimia 30 ikibaki kutokana na ukosefu wa fedha, na kwamba awamu ya tatu itawatambua walengwa wote kwa asilimia 100.**

# Polisi yapiga 'stop' maandamano mtandao

**Fatma Mtutuma na Faudhia Sultan, UDOM**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limetoa onyo kwa watu wanaopanga kufanya maandamano leo (Julai 7) kwa ajili ya kudai Tume Huru ya Uchaguzi (NEC).

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini humo, Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alisema watu watakaofanya maandamano hayo watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

"Jeshi linatoa onyo kali kwa kikundi au mtu yeyote atakayeshiriki maandamano hayo batili Julai 7 kwa madai ya kudai Tume Huru ya Uchaguzi, waache mara moja vinginevyo watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria," alisema Mambosasa.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, (KKKT) Dayosisi ya Karagwe Kagera, Dk. Benson Bagonza, alisikika hivi karibuni akiunga mkono wazo la kufanyika kwa maandamano hayo kwajili ya kudai Tume Huru ya Uchaguzi na kuungwa mkono pia na baadhi ya watu hasa watumiaji wa mtandao wa Twitter.

Watu hao walianzisha kampeni ya '77 nyeupe' kwa aiili ya kuhamasisha wananchi wenye nia ya kudai tume hiyo kuvaa nguo nyeupe kama ishara ya kudai haki hiyo kwa siku ya leo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe (kulia), akizungumza kwenye kikao kazi na watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kulia) ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Katibu Mkuu UPDP ajitosa urais Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha UPDP, kimeanza rasmi mchakato wa kumtafuta mgombea urais wa Zanzibar, ambapo Katibu Mkuu wake Taifa, Hamad Mohamed Ibrahim (pichani), amejitokeza kuchukua fomu ya kuwania nafasi hiyo.

Uchukuaji wa fomu ulifanyika katika ofisi za chama hicho Mtoni Kidatu Mjini Unguja, na alikabidhiwa fomu na Mjumbe wa Halmashauri kuu na Mkurugenzi wa Uchaguzi, Barik Ali Omar.

Baada ya kukabidhiwa, Ibrahim alisema kwamba kilichomsukuma kuchukua fomu ni Katiba ya Zanzibar ambapo inaruhusu kila baada ya miaka mitano vyama kushiriki katika uchaguzi.

"Ndugu zangu wanahabari, nimejitokeza kuchukua fomu ya kuomba chama changu kinichagüe niwe mgombea wa nafasi ya urais ... haimaanishi Serikali iliyokuwa madarakani haijafanya kitu, bali nimekamilisha malengo ya chama chetu



na chama chochote cha siasa kukamata dola," alisema Ibrahim.

Alisema Serikali inayomaliza muda wake imejitahidi kwa kiasi kikubwa kufanya mengi mazuri kwa maslah mapana ya wananchi kwa kuboresha huduma mbalimbali za kijamii.

Alisema endapo chama chake kitampa ridhaa ya kuwa mgombea urais na wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba wakamamchagua kuwa Rais wa Zanzibar, ataendeleza yale yote mazuri ambayo yamefanywa na Serikali inayomaliza muda wake.

"UPDP imeshaonyesha njia ya kutaka kuongoza nchi hii, tutaendeleza yale yote mazuri ambapo serikali hii imeanza kuyafanya na kwenda mbali zaidi kutoka katika uchumi wa kati ambao tumeingia hivi sasa na kwenda katika uchumi wa juu zaidi," alisema Ibnrahim.

Hata hivyo aliahidi kuboresha miondombinu ya barabara pamoja na kuboresha huduma muhimu za kijamii kama majisafi na salama pamoja na huduma zaa kwa wanachi. Alisema pia atahakikisha anatatua changamoto ya udhalilishaji ambayo kwa sasa inavitafuna visiwa hivyo.

Naye Barik Ali Omar alisema uchukuaji wa fomu uko wazi kwa wanachama wote ambapo wanahisi wana uwezo wa kugombea nafasi yoyote ndani ya chama hicho wajitokeze, na kwamba wanaendesha zoezi hilo kwa kuzingatia demokrasia wala ubaguzi.

## Corona yawaepusha vijana 100 kwenda gerezani

**Na Hellen Mwango**

VIJANA Watanzania 100 wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za kuondoka nchini kinyume cha sheria na kuzamia Afrika Kusini bila kufuata taratibu za Idara ya Uhamiaji.

Watuhumiwa hao wamesomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Washtakiwa waliposomewa mashtaka yao wamekiri kutenda kosa hilo na wameiomba mahakama iwasamehe.

Hata hivyo, Hakimu Simba alisema kuwa haoni faida yoyote ya kuwapeleka watuhumiwa hao gerezani hasa katika kipindi hiki cha hatari ya ugonjwa wa corona.

"Mahakama yangu inaona hakuna faida yoyote ya kuwapeleka gerezani, lakini inawapa onyo kali na inawaachia kwa masharti msirudie kutenda kosa hili kwa miezi sita," alisema Hakimu Simba.

Mwendesha Mashtaka wa Idara ya Uhamiaji, Godfrey Ngwijo, alidai kuwa Julai 3, mwaka huu katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote 100 wanadaiwa kuondoka nchini kwenda Afrika Kusini, kinyume cha sheria bila kufuata utaratibu.

Wakisomewa maelezo ya awali imedaiwa katika tarehe zisizojulikana washtakiwa hao waliondoka nchini bila kufuata utaratibu na kwamba Julai 3, mwaka huu watuhumiwa walirudishwa nchini baada ya uchunguzi na kugundulika kuwa ni wahamiaji haramu.

## WLAC yaanzisha elimu utafutaji haki

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC), kimeanzisha mpango wa kuelimisha na kuhimiza jamii kutambua haki zao zilizopo kisheria, kwa lengo la kuboresha na kuhamasisha jamii kutafuta msaada wa kisheria pale wanapokosa haki.

Mkurugenzi Mtendaji wa WLAC, Theodosia Muhulo, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akizindua mpango huo wa miaka miwili unaofadhliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Tanzania (LSF).

Alisema mpango huo unawalenga zaidi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema makundi mengine yatakayoyafikiwa ni ya wanachama wa vyama vya wafanyakazi, vyama vya waajiri na maofisa wanaofanya kazi katika wilaya zote za mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema lengo ni kuwasaidia kupigania haki zao za msingi ikiwamo kupambana na ubaguzi katika maeneo yao ya kazi.

Muhulo alisema wameamua kuanzisha mpango huo baada ya ofisi yao kuendelea kupokea kesi nyingi za wafanyakazi zinazotokana na matatizo katika maeneo wanakofanyia kazi na wanaamini utawafikia wafanyakazi wengi na kusaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza changamoto hiyo.

HABARI KITAIFA

## Mtuhumiwa mauaji, ubakaji mwanafunzi akamatwa

**Na Said Hamdani, LINDI**

JESHI la Polisi Mkoani Lindi, linamshikilia mkazi wa Kata ya Mnolela, Salum Miheva (34), kwa tuhuma za kumuua mwananchi mwenzake Issa Selemani (62) kwa kumkata mapanga shingoni, alipokuwa akimwokoa mwanafunzi aliyekuwa akibakwa na mtuhumiwa miaka miwili iliyopita.

Mtuhumiwa anadaiwa kufanya unyama huo Novemba 17, 2018 katika misitu ya mashamba yaliyopo katani humo kisha kutoroka na kujificha mashambani mwa kijiji cha Mbuta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Stanley Kulyamo, alisema juzi kuwa mauaji hayo yalifanyika wakati mwanafunzi huyo akiwa anarejea nyumbani kutoka shuleni.

Alisema wakati mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) anarejea nyumbani, njiani alikutana na mtuhumiwa ambaye alimkamata na kumvutia kichakani kasha kumbaka.

Kuyamo allisema wakati mtuhumiwa akitekeleza unyama huo, Selemani, ambaye sasa ni marehemu, akiwa anakwenda shambani alisikia kelele za mtoto huyo akiomba msaada na alipofuatilia alimkuta mtuhumiwa akimbaka na alipomsogelea ili kutoa msaada, alikatwa na panga shingoni.

Alisema Selemani alifariki dunia akiwa njiani kupelekwa hospitali ya Nyangao kwa matibabu baada ya kutokwa na damu nyingi na mtuhumiwa alitoroka baada ya kufanya tukio na kukamatwa mwaka huu akiwa amejificha katika mashamba ya Kijiji cha Mbuta.

Kamanda Kuyamo alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabiri baada ya kukamilika kwa uchunguzi na taratibu zingine.

**Kuyamo allisema wakati mtuhumiwa akitekeleza unyama huo, Selemani, ambaye sasa ni marehemu, akiwa anakwenda shambani alisikia kelele za mtoto huyo akiomba msaada na alipofuatilia alimkuta mtuhumiwa akimbaka na alipomsogelea ili kutoa msaada, alikatwa na panga shingoni.**

# Majaliwa asisitiza udhibiti fedha za umma

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa alisema serikali itaendelea kudhibiti matumizi ya fedha za umma ili kuendelea na ujenzi wa miradi ya kimkakati zikiwamo bandari kwa lengo la kuboresha maendeleo ya wananchi.

Pia amesema changamoto ya usafirishaji wa mizigo na abiria kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) itakuwa historia baada ya kuboreshwa na kujengwa kwa miundombinu ya bandari katika ukanda wa Ziwa Tanganyika ukiwamo upanuzi wa bandari ya Kasanga.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi katika mradi wa upanuzi wa bandari ya Kasanga, wilayani Kalambo akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Rukwa. Mradi huo unagharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.7.

Alisema upanuzi wa bandari hiyo utawezesha mizigo inayotoka nchini kwenda Congo kufika kwa wakati kwa sababu itasafirishwa moja kwa moja bila kupitia katika nchi nyingine kama ilivyo sasa, ambapo madereva wanalazimika kupita kwenye mataifa mengine na kutumia muda mrefu.

"Mradi huu ukikamilika utaongeza pato la mwananchi mmoja mmoja pamoja na taifa kwa ujumla. Rais John Magufuli amedhamiria kuboresha maendeleo ya wananchi nchi nzima ikiwamo na wilaya hii ya Kalambo. Ujenzi wa miradi hii unatoa fursa za ajira kwa wananchi, hivyo zichangamkieni," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema mapambano dhidi ya rushwa bado yanaendelea nchini, hivyo mtu yeyote atakayebainika anajihusisha na masuala hayo atafutwe popote alipo, akamatwe na achukuliwe hatua za kisheria.

Sambamba na hilo, aliwakumbusha watendaji ndani ya serikali wahakikishe wananchi wanapofika katika maeneo yao ya kazi wawapokee, wawasikilize na kuwahudumia bila ubaguzi.

"Hatuangalii sura wala kabila. Yeyote atakayekanyaga kwenye maeneo yenu ahudumiwe ipasavyo," alisema.

Naye Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema Tanzania na Congo zimeungana kwa Ziwa Tanganyika lakini usafiri wa barabara uliokuwa unatumika awali uliyalazimu maroli ya mizigo kupitia nchini nyingine na kuchelewa kufika.

Alisema kukamilika kwa upanuzi wa bandari hiyo pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwago cha lami kutoka Sumbawanga hadi Kasanga, kutarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia bandari hiyo kuingia nchini Congo moja kwa moja bila kupita nchi jirani.

Waziri Kamwelwe alisema awali kulikuwa na changamoto ya barabara hali iliyosababisha meli kufika kwenye Bandari ya Kasanga na kulazimika kusibiri mizigo ambayo ilikuwa ikichelewa kufika kutokana na ubovu wa barabara na sasa tayari serikali imetatua kwa kujenga kwa kiwango cha lami.



Kaimu Mkurugenzi Elimu ya Ufundi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Margaret Mussai, akifunga mafunzo ya ufundishaji kwa njia ya masafa kwa walimu wa vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDCs), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi wa Shirika la Karibu Tanzania Organization (KTO), Maggid Mjengwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jamii yatakiwa kulinda misitu

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, ametoa wito kwa jamii, kushirikiana na serikali katika kulinda na kuhifadhi misitu kwa ajili ya faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

Dk. Nzuki alitoa wito huo alipotembelea banda la Wizara ya Maliasili na Utalii kujionea shughuli mbalimbali zinazoendelea katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika viwanja vya Julius Nyerere.

Alisema misitu ni sekta muhimu ambayo inategemewa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, hivyo kuna haja ya kuendelea kuitunza na kuilinda.

Aliupongeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa shughuli inazozifanya za kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa misitu, uendelezaji utalii ikologia na malikale.

Dk. Nzuki alisema ameridhishwa na namna TFS ilivyojipanga katika maonyesho hayo na kuiagiza kuendelea kuboresha zaidi ikiwamo kufanyia kazi mapendekezo wanayopewa.

"Nimefurahishwa kuona shughuli zote mnazofanya ziko bandani hapa, nimepata historia nzuri ya michoro ya Kondoa Irangi, Hifadhi za Mazingira Amani ziko hapa zikiwakilishwa na hifadhi mama ya Amani, lakini kurugenzi ya uzalishaji mbegu za miti imeimarika na wanatoa mbegu na miche bora ya matunda na miti kwa wananchi," alisema Dk. Nzuki.

"Hakika mmejipanga na hata nimeshuhudia jinsi mlivyojipanga kupambana na moto kupitia satelaiti ya kufuatilia majanga ya moto. Nitoe wito kwa jamii kuungana na serikali kulinda na kuhifadhi misitu, serikali inatimiza wajibu wake na naomba wananchi nao washiriki katika kuhifadhi maliasili zilizopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho."

Kaimu Meneja wa Mawasiliano TFS, Martha Chassama, alimhakikishia Dk. Nzuki kuendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii namna ya kulinda, kuhifadhi na kutunza hifadhi za misitu.

## Walalamikia kuondolewa maeneo ya biashara

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

WAFANYABIASHARA wadogo katika mabanda ya soko kuu, stendi kuu na stendi ya mabasi ya vijijini katika Kata ya Nanjoka, Tunduru mkoani Ruvuma wamelalamikia tamko la Halmashauri linalowataka kuondoka katika vibanda wanavyofanyia biashara.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa masharti ya kutotaja majina yao, walisema malalamiko hayo yametokana na halmashauri kuchukua hatua hizo bila kuwahusisha wafanyabiashara hao ambao ndio waliojenga mabanda hayo kama sehamu ya hamasa ya kuendeleza eneo hilo.

Kwa mujibu wa wafanyabiashara hao, kabla ya kujenga mabanda hayo, eneo hilo halikuwa na kitu chochote lakini baada ya kukamilisha ujenzi huo, halmashauri imeingilia kati na kuanza kuwatoza pango huku kukiwa hakuna makubaliano yoyote.

Akizungumzia sakata hilo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Ofisa Mapato wa Halmashauri hiyo, Obeth Mwakisole, alisema tozo ya pango inategemea ukubwa wa chumba.

Mwakasole alisema katika mkataba wa upangishaji kuna kipengele kinachomwelekeza mmiliki wa vibanda hivyo ambaye ni halmashauri, kufanya ukaguzi ili kubaini matukio mbalimbali yanayoendelea katika maeneo hayo.

Alisema kimsingi halmashauri inamtaka mmiliki wa kibanda husika awe na leseni ya biashara anayofanya kwenye chumba husika lakini sehemu kubwa ya vibanda vilivyopo katika maeneo ya stendi, soko kuu na stendi ya mabasi ya vijijini, vinamilikiwa na watu ambao hawafanyi biashara.

Kwa mujibu wa Mwakasole, kazi ya kubaini uwapo wa wafanyabiashara wanaopangisha vibanda hivyo ilifanywa na tume ambayo iliundwa na mkuu wa wilaya baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wanaoendesha shughuli zao katika mabada hayo kuwa wamekuwa wakitozwa kodi kubwa ya pango na watu wanaojiita wamiliki wa vibanda hivyo.

"Ni tabia tu ya watu wajanja kutaka kupata fedha kwa njia isiyokuwa halali. Wanakiuka taratibu za ununuzi. Kumekuwa na watu ambao hufikia hatua hata kuuziana mabanda hayo huku wakiwa hawakuyajenga wao," alisema Mwakisole.

Alisema lengo la halmashauri ni kumfanya mwananchi wa Tunduru anayefanya biashara katika maeneo hayo kupata faida kubwa ikiwa ni tofauti na wafanyabiashara ambao wamepanga katika mabanda yaliyoko nje ya vibanda vya halmashauri ambao wanatozwa pango kubwa na kuwafanya wapate faida ndogo.

# Wanafunzi wenye uhitaji maalum wakwama kurudi shule

**Na Zuwena Shame, IRAMBA**

JANGA la virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19 limekuwa changamoto kwa baadhi ya wanafunzi wenye uhitaji maalum kurudi shuleni na kuhudhuria masomo baada ya shule kufunguliwa.

Shule ya Msingi Kizega iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida, ambayo ni mchanganyiko wa watoto wenye uhitaji maalumu, tangu ilipofunguliwa mwanzoni mwa wiki iliyopita ni asilimia 40 pekee ya watoto hao ambao wameripoti shuleni na ina jumla ya watoto 50 wenye uhitaji maalum.

Wengi wa watoto hao wanatoka vijijini vya jirani wilayani humo kama Shelui, Igugumo, Nduguti, Tuliya na Ivugu.

Wanafunzi hao wengi hawawezi kwenda shuleni bila msaada wa wasaidizi walio waaminifu kwa ajili ya usalama wao wawapo njiani.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Andrea Nyoni, alisema watoto wengi wana changamoto ya usafiri na kushindwa kufika shule kwa muda uliopangwa.

"Wengi wao wana changamoto ya usafiri maana wanatoka mbali na hivyo wanakaa hapa shuleni kama wanafunzi wa bweni ili kupata uangalizi zaidi. Hawawezi kwenda na kurudi kutokana na hali zao," alisema Nyoni.

Msimamizi wa watoto hao shuleni, Grace Samson, alisema corona imewakwamisha wazazi wengi kuwapeleka watoto shule baada ya kufunguliwa kwa kuwa shughuli zao za kiuchumi zilikwama na wengi wanatoka mbali na hivyo vipato vyao kuwa duni na kukosa fedha kwa ajili ya nauli.

Alisema sio kawaida ya wazazi hao kuchelewesha kuwarudisha watoto shuleni na wengi wao walipoulizwa walisema vipato vyao vimekuwa duni kutokana na corona.

Samson aliiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwarudisha shule na kuwarudisha nyumbani kipindi cha likizo kubwa kwa kuwa wazazi hawawezi kumudu gharama za usafiri.

Alisema kutokana na hali zao hata baadhi ya walezi na wazazi wanaona usumbufu kuwapeleka shule na matokeo yake watoto hao wanakosa elimu ambayo ndio msingi wa maisha yao.

Kadhalika alisema, changamoto nyingine inayowakabili wanafunzi hao ni ukosefu wa sabuni za kufulia vitambaa vya hedhi kwa wasichana.

Alipoulizwa na Nipashe kuhusu sababu ya kutomrudisha mtoto shuleni baada ya kufunguliwa, mlezi wa mtoto mwenye ualbino kutoka Kijiji Cha Igugumo, Ramadhani Hamisi (32), alisema fedha imekuwa changamoto hasa kipindi hiki cha ugonjwa wa corona kwa kuwa anategemea kuuza nafaka kwenye magulio na minada ili kujiingizia kipato na kumhudumia mwanawe.

Hamisi alisema kuwa kutokana na janga hilo wafanyabiashara kutoka mjini hawaendi vijijini kununua bidhaa hivyo kufanya maisha kuwa magumu na kushindwa kuhudumia familia.

Alisema pia mtoto wake hana sare za shule na begi, hali inayomfanya ashindwe kumpeleka shuleni.

"Uwezo wangu ni mdogo, hivyo naendelea kudunduliza niweze kumnunulia mahitaji muhimu nimrudishe shuleni pengine wiki ijayo," alisema Hamisi.

Alipoulizwa kuhusu changamoto hiyo, Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Chacha Kehogo, alikiri kuwapo na amemuagiza Ofisa Elimu Maalumu kwenda shuleni hapo kujua matatizo ya wanafunzi hao ili warudishwe shuleni.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT), jumuiya ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Kisukuru, Mery Mdegipala, akifungua kikao cha wanawake wa chama hicho, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ili kuwahamasisha na kuwatia moyo wa kushiriki kugombea nafasi za Udiwani na Ubunge katika uchaguzi mkuu ujao. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Watamba kukubaliana na corona

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

BAADHI ya shule za msingi na sekondari Tunduru mkoani Ruvuma, zimetamba kujizatiti katika utekelezaji wa maelekezo ya kuwakinga watoto dhidi ya corona.

Hayo yalibainishwa na Mwalimu Esther Mkami wa Shule ya Msingi Nanjoka kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wameripoti shuleni kwa sasa na walimu wa madarasa wanazingatia kuchukua tahadhari juu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Nao baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walisema kwa sasa wanafunzi wote wako makini na wanazingatia maelekezo ya kunawa maji tiririka na sabuni pamoja na kukaa mbalimbali hata wakati wa kucheza.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Nanjoka, Ausi Chimsala, alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,446 na darasa la saba wako 133 ambao wako katika mkondo mmoja ikiwa ni tofauti na maelekezo ya serikali kwamba kila darasa wakae watoto 45 kwa kila chumba.

Alisema hali hiyo inatokana na shule hiyo kukabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa. Alisema mahitaji ya vyumba vya madarasa katika shule hiyo ni 26 wakati yaliyopo ni 13.

Changamoto kubwa katika shule yake ni uwepo wa upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo ambapo kwa idadi hiyo ya wanafunzi waliopo wanahitaji matundu ya vyoo 64 yaliyopo 28 na upungufu ni 36 hali iliyopelekea kuwagawa katika makundi matatu na kuwafungishia katika madarasa ya mda nje ya eneo la shule.

Katika Shule ya Sekondari Frank Weston, Mwalimu Amuli Hamza alisema shughuli zote zinaendelea vizuri kutokana na shule yao kuandaa matangi yenye maji tiririka na matumizi ya barakoa kwa wanafunzi.

Nao wanafunzi Shabani Chikambo na Zurfa Selemani waliwapongeza wazazi wao kwa kukubali kujitolea kuchangia chakula hali ambayo itawafanya kula chakula shuleni na kuwahakikishia utulivu wa akili.

Walisema kabla ya hapo, wakati wa masomo walikuwa wanakaa muda mrefu bila kupata masomo kutokana na janga la kirusi cha corona.



Ukurasa 12

## Waliotumia mikorogo utotoni ukubwani waangukia majuto



Ukurasa 14

**Ni wakati wa kufundishana kukataa ‘chai’ ya uchaguzi**



Ukurasa 13

Ondoa fikra za ‘ni mwaka wa fedha’ uchague kiongozi bora

TEKNELOJIA

NA AGNES TEMU

# Je wajua, injini gesi asilia ni ‘kiboko’ kuliko ya petroli?

• Mara mbili ya uwezo wa petroli




Moja ya magari ya injini ya gesi. **PICHA: MTANDAO**

MABADILIKO ya kiteknolojia kwenye injini za magari ambazo badala ya kutumia mafuta huendeshwa kwa gesi asilia, huenda yakawashawishi Watanzania wengi kutumia gesi kwani hupunguza gharama ikilinganishwa na zile za dizeli na petroli zinazogharimu zaidi.

Ili kutimiza azma hiyo, taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kwa kushirikiana na wadau inaunganisha mfumo wa gesi asilia kwenye magari yanayotumia petroli.

Kubadili mfumo huo hufanywa kwa magari madogo hadi makubwa na mpaka sasa zaidi ya magari 350 yako barabarini yakitumia gesi asilia, kwa mujibu wa Mratibu wa Gesi Asilia wa DIT, Dk.Esebi Nyari.

Anaeleza kuwa wateja wakubwa wa teknolojia hiyo ni kampuni ya kigeni ya Uber. Anafafanua Nyari kuwa, gharama za kuweka mfumo wa gesi asilia hutegemeana na aina au ukubwa wa gari.

Katika mahojiano na Nipashe, anaeleza kuwa magari mengi madogo yenye ‘silinda nne’ ni Sh. 1,800,000 wakati silinda sita gharama ya kubadilisha mfumo wake ni 2,200,000 na hutoza Sh. 2,500,000.

“Hata hivyo, gharama hii inaweza kurudishwa mapema zaidi kutokana na matumizi na unafuu wa gesi asilia.” Anasema Dk. Nyari.

### FAIDA GESI ASILIA

Faida za matumizi ya gesi asilia kwenye magari ni nyingi na anataja kuwa bei ya gesi ni nafuu na rahisi zaidi kwa asilimia 45 ikilinganishwa na petroli.

Aidha, anaeleza kuwa kilo moja ya gesi asilia kwa sasa ni Sh. 1,550 ikilinganishwa na petrol ambayo ni 2,100 kwa lita.

“Gesi hiyo utaitumia kusafiri zaidi ya kilometa 20 ukilinganisha na petrol ambayo inasafiri kilometa 12 kwa lita.” Anaeleza Mratibu wa Gesi Asilia wa DIT.

Aidha, gesi asilia ni safi ukilinganisha na mafuta mengine kama petroli au dizeli, hivyo kutumia gesi asilia kwenye gari kunapunguza uchafuzi wa mazingira, injini na afya za watumia barabara. Anazungumzia gharama za matengenezo wa magari zinapunguzwa endapo mmiliki anatumia gesi asilia.

“ Hii ni kwa sababu gesi asilia ni safi na muwako wake hauna masizi au kaboni, ukilinganisha na mafuta, hivyo itachukua muda mrefu kufanya ukarabati wa gari linalotumia gesi asilia. Litafanyiwa matengenezo baada ya kutembea kilomita 6,000 ikilinganishwa na gari linalotumia mafuta linalifanyiwa matengenezo baada ya kilomita 3,000.”

### CHANGAMOTO

Dokta Nyari anabainisha kuwa, licha ya mafanikio ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari, changamoto kubwa za mradi huu ni uhaba wa vituo vya kujazia gesi, wataalamu wachache wa mambo ya gesi asilia na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu nishati hiyo.

Anaeleza kuwa serikali kupitia taasisi zake imekuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto hizi kadri muda na rasilimali fedha zinavyopatikana. Mfano, Shirika la Maendeleo ya Mafuta (TPDC) limetangaza kampuni zinazoonyesha nia ya kuwekeza kwenye eneo hilo hapa nchini wakiwamo wazawa.

Anaamini muda si mrefu vituo vya kujazia gesi vitaongezeka nchini.

### KUELIMISHA JAMII

Kwa upande mwingine, Taasisi ya DIT imekuwa msitari wa mbele kuelemisha wananchi masuala ya gesi.Dokta Nyari, anaeleza: “Ili kufikia watu wengi kwenye biashara ya gesi asilia DIT imekuja na mpango kazi wa kufanya mafunzo ya muda mfupi ili kuongeza idadi ya mafundi wenye uwezo wa kufunga mfumo wa gesi asilia kwenye magari.”

Anasema mafunzo haya yalitarajiwa kuanza mwezi ujao lakini kutokana na ugonjwa wa corona yamesogezwa mbele.

### MAONI YA WATEJA

Akiongea na Nipashe, dereva wa Uber, anayefanya safari zake Dar Es Salaam, Leonard Kitenga, anasema kuwa faida ya kutumia gesi ni kubwa kutokana na kupunguza gharama.

Anasema ikiwa anatumia gesi ya Sh. 100,000 utapata faida ya 50,000 kwa siku pia matengenezo ni nafuu zaidi.

Mfanyakazi wa kituo kinachojaza mafuta kilichoko Ubungo, anasema kuwa wateja wanaoweka gesi wanawakagua ili kuangalia iwapo muda wa matumizi umekwisha au lah.

Anasema hatoi gesi kwenye mitungi isiyofungwa kwenye magari, hawauzi bila kukagua stika za muda wa matumizi ili kuepusha mlipuko na kusababisha ajali za moto wa gesi,”anaeleza mfanyakazi huyo jina tunalo.

### MWANZO WA UTAFITI

Mradi wa gesi asilia inayotumika kwenye magari ulifanyiwa majaribio kwa miaka kumi 11, kazi ikianza mwaka 2009 mpaka mwaka huu.

Utafiti umeonyesha mafanikio kwa kuongeza ajira kutoka watu wawili hadi 3,000 sasa.

Mkufunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Hassan Rajabu, ndiye anayeeleza mafanikio ambayo yamepatikana kwa muda wa miaka hiyo tangu kubainika kwani gesi asilia nchini.

Dokta Rajabu anasema kuwa mwaka 2009 mradi wa majaribio ya kufunga gesi kwenye magari ulianza lakini ulikumbwa na changamoto lukuki na kusimamishwa.

Anasema ilipofika mwaka 2018 ulianza tena na mafanikio yalionekana hadi sasa na kwamba tatizo kubwa ni upungufu wa wataalamu ikiwamo wa kukagua mfumo wa kufunga gesi kwenye magari ili kuepusha ajali na magari kuteketea.

Anasema wakati mwingine kuna changamoto ya madereva ambao baada ya kufungiwa mfumo wa gesi, huuza na kufunga mtungi kwenye gari jingine bila kuwasiliana na DIT.

Anasema kutokana na watumiaji kutokuwa na uelewa wa mfumo wanajiweka katika hatari .

Anakumbusha kuwa inatakiwa gari likianza kutoa moshi watumiaji wakae umbali wa mita 200 ili kuepuka madhara ya mtungi kulipuka na kupaa.

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

# Waliotumia mikorogo utotoni ukubwani waangukia majuto

## •Weupe wa 'dukani' unawataabisha

KARISHMA Leckraz, Anusha na Sabrina Manku wote wametumia bidhaa za kujichubua. Karishma alianza mkorogo ili kuupata weupe akiwa na umri wa miaka 13 baada ya kuarifiwa kwamba atakuwa mzuri zaidi na ngozi yake itang'ara.

"Niliambiwa kwamba nina umbo zuri , lakini ni aibu kwasababu ni mweusi mno," anasema msichana huyo ambaye sasa ana miaka 27.

Anaeleza kuwa alifundishwa na wazazi kutumia 'mkorogo' kujichubua wakitaka awe mweupe. Anasimulia "Mizizi ya utamaduni wetu imejikita kwenye dhana kuwa ukiwa mweupe wewe ni mzuri."

Ni aina ya utamaduni unaopatikana ukanda wa Asia ya Kusini, ambako ngozi nyeupe inachukuliwa kuwa nafsi bora.

Lakini, hivi karibuni kuna mageuzi ya kimtazamo, mjadala unaotawala baada ya kifo cha George Floyd , Mmarekani mweuzi aliyeuawa kwa kukandamizwa shingoni na polisi mweupe, umezaa mtazamo mpya.

Kampuni ya Unilver, inayozalisha sabuni na vipodozi imesema itaacha kutumia neno 'fair (ngozi bora) kwa krimu za usoni inazotengeneza kumchubua mtu awe mweupe nchini India na kubadilisha nembo yao ikiitwa 'glow and lovely' ikimaanisha 'ung'avu unaopendeka.'

Karishma ni msanii wa urembo anayeendeleza ujumbe chanya kuhusu ngozi asilia ya mtu akisema krimu alizotumia utotoni, zilimuongezea vipele usoni. Karishma aliacha kupiga picha na rafiki zake akiwa kijana.

"Sikutaka nionekane kwenye picha jinsi nilivyo mweusi. Nilifuata kile watu maarufu walichofanya'," anasimulia


'Usikae juani kwa muda mrefu' kama Karishma, Sabrina Manku anakumbusha alivyoambiwa na familia yake kwamba yeye ni mweusi sana.

### SABRINA NA YAKE

Huko jimboni Punjabi nchini India, kwa mujibu wa Sabrina falsafa hiyo kuhusu rangi ya mabinti, imetawala imani hata kufikia kiwango cha kuweza kuwaumiza roho , panapokuwapo jambo linalokwenda kinyume na mtizamo huo.

Hapo Sabrina anarudisha kumbukumbu mbali zaidi, yungali binti mdogo wa miaka 10, alipoonyeshwa krimu hizo za kujichubua alizozitumia kwa miaka minane.

Leo hii, Sabrina anayesoma sheria katika Chuo Kikuu cha Leicester nchini Uingereza, anasema alipata mabadiliko ya kifalsafa yaliyompa ujasiri na kujiamini, kwa rangi yake ya asili, pia umbo lake, akiweka kando mtizamo wa familia.



Athari za mkorogo zinavyoumiza watu na kusababisha hasara nyingi kiafya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Sio kila mmoja anayenunua bidhaa ya kumbadilisha rangi anataka awe mweupe milele. Kwangu mimi, ngozi yangu inaonekana kung'aa inapokuwa imekolea.



Ngozi nyeusi inapigwa vita na weusi kulazimishwa kutumia mikorogo kuwa weupe.

Mwanamke mwingine anayejitambulisha kwa jina moja la Anusha, anasema imani za kuendekeza kutumia 'mikorogo' mzizi wake si kwenye familia pekee, bali nje ya maisha ya hapo akirejea nafasi yake binafsi kwamba aliipatia shuleni kuwa 'mwana-mkorogo' kupitiliza.

Anakumbusha alivyoanza kujenga tabia hiyo akisimulia kwamba: "Nilijiona nikianza kujilinganisha na watu ambao walikuwa weupe.

"Wasichana maarufu wangechukuliwa na watu tofauti si kwa jambo lingine zaidi tu ya rangi ya ngozi yao nyeupe."

Sabrina anazungumzia Bollywood, ambayo ni tasnia ya filamu nchini India, ilivyomshawishi hata akazamia zaidi kutumia krimu zilizomchubua ngozi.

"Niliangalia waigizaji nyota na kufuata mitindo yao, chochote ambacho wamezindua," anaeleza kuhusu nyota wa Bollywood, ambao sasa wanakosolewa kwa kutangaza bidhaa zinazoendekeza kujichubua.

Msanii huyo anaendeleza ufafanuzi wake kuwa:"Inakufanya tu uhisi wewe ngozi yako ni nyeusi na kutumia bidhaa fulani kutafanya ubadilike kwasababu waigizaji nyota wanakuambia kwamba utaona mabadiliko."

Anasema, baadhi ya matangazo ya biashara yamechangia, yakiwamo yanayohusu wanaume kuvutiwa na wanawake weupe, baada ya kuanza kutumia bidhaa za mkorogo wakati awali walikuwa weusi.

"Nilitaka kuwa mwanamitindo. Lakini kila wakati nilifikiria kuwa ngozi yangu nyeusi itanifanya nisipate kazi," anarejea alivyoguswa.

"Nimebaini kwenye filamu kuwa na ngozi nyeupe kunachukuliwa kuwa mzuri zaidi. Nilitaka kuonekana kama wale ninao waona kwenye televisheni," Sabrina anaongeza.

### WALIVYOBADILI

Karishma na Sabrina leo hii , si watumiaji tena wa bidhaa hizo za kubadili rangi na wanatoa sababu kuu mbili; wanafahamu athari zilizoko na wanajiamini zaidi.

Wanarejea msingi wa hoja zao, kwamba familia na shinikizo la jamii ndiyo imewafikisha hapo kwenye kujichubua lakini sasa hivi hali imekuwa tofauti.

"Sio kila mmoja anayenunua bidhaa ya kumbadilisha rangi anataka awe mweupe milele. Kwangu mimi, ngozi yangu inaonekana kung'aa inapokuwa imekolea.

Anusha anaeleza kuwa mwenendo wake wa leo hii ni kwamba, anatumia bidhaa za urembo za 'mask' ambazo zinabadilisha ngozi yake iwe nyeupe.

Kwa mujibu wa mtizamo wake ni kwamba, tabia zote alizonazo sasa kuhusu kujichubua na kubadili rangi ya ngozi , ni zao linalotokana na alichofunzwa utotoni

***•Kwa mujibu wa BBC***

ELIMU

**NA REUBENI LUMBAGALA**

# Ondoa fikra za 'ni mwaka wa fedha' uchague kiongozi bora

OKTOBA mwaka huu, Tanzania inatarajia kufanya uchaguzi mkuu kuchagua viongozi kwa nafasi ya rais, wabunge na madiwani.

Hili ni tukio muhimu katika historia ya nchi hii kwani uchaguzi ni mfumo wa kidemokrasia ambao wapigakura wanapata fursa ya kuingia mkataba na viongozi wanaogombea nafasi mbalimbali za uongozi kupitia sanduku la kura.

Lengo ni kufanikisha jitihada za kujiletea maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa nia ya kuleta ustawi bora wa maisha ya wananchi.

Ndani ya vyama vingi vya siasa, pazia la kutangaza nia limefunguliwa rasmi ambako wagombea wanatangaza kutia nia kugombea nafasi mbalimbali ili vyama vyao viwapatie ridhaa ya kugombea na hatimaye waweze kuwatumikia wananchi.

Pamoja na ari ya dhati waliyonayo baadhi ya wagombea kuwatumikia wananchi, rushwa ni kikwazo cha kutimiza matarajio ya wananchi ya kupata viongozi bora kwa ajili ya kusukuma gurudumu la maendeleo.

Kama nchi; serikali na wananchi au wapiga kwa ujumla wana wajibu wa kushiriki moja kwa moja kuhakikisha kuwa vitendo vya rushwa katika uchaguzi mkuu vinadhibitiwa ili kutimiza kiu ya wananchi ya kupata viongozi bora wa kuwaongoza kwa miaka mitano ijayo kuanzia 2020 hadi 2025 utakapofanyika mwingine.

Siyo siri inafahamika rushwa ni adui wa haki, penye rushwa, lazima pawepo kupindishwa taratibu, sharia na kuwanyima wananchi haki na stahili yao.

Rushwa ni tatizo ambalo linahusisha pande mbili; upande wa anayetoa na mwingine anayepokea au kinyume chake. Kwa mantiki hii anayetoa na anayepokea rushwa, wote wanafanya kosa kwa mujibu wa sheria za nchi hii.

Kwa muktadha wa uchaguzi, mtoa chai au takrima huwa ni mgombea wa nafasi ya uongozi au wapambe wa mgombea na mpokeaji huwa ni mwananchi au mpigakura.

Inasikitisha kuona baadhi ya wagombea kabla ya kutinga uliongoni hujipanga kwa kiwango kikubwa katika bajeti ya rasilimali fedha ili kuwahonga wapiga kura kabla hata kufikiria namna bora anayoweza kuwatumikia wananchi na kusaidia ustawi bora wa jimbo analotaka kuliongoza.

Miongoni mwa sifa za msingi za kiongozi bora ni yule anayechukia kwa vitendo rushwa, hivyo hujiepusha kutoa rushwa ili aweze kuchaguliwa na wananchi.

Kama mbunge au diwani ana uhakika wa weledi, sifa na uwezo wa kuwatumikia wananchi, ana haja gani ya kutoa rushwa? Utoaji rushwa ili kupata nafasi ya uongozi ni kutojiamini, ni kukosa sifa ya kuwatumia wananchi na kupoteza haki.

Tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu, wananchi waachane na dhana potofu kuwa huu ni mwaka wa kuvuna fedha kutoka kwa wagombea.

Hakuna fedha yenye thamani ya kura ya mwananchi wala uwezo wa kutatua shida binafsi za wapigakura.

Pamoja na makosa yanayofanywa na baadhi ya wagombea kutoa rushwa ili kuchaguliwa, kwa upande mwingine wananchi na wapiga kura ni sehemu ya tatizo hili la rushwa kwenye uchaguzi, kutokana na ushiriki wao katika kuomba au kupokea rushwa kutoka kwa wagombea.

Hivyo, ili kumaliza tatizo hili, wananchi wawe mstari wa mbele kukataa kupokea rushwa na kumuadhibu mgombea anayetoa rushwa kwa kumnyima kura na kuripoti vitendo hivi katika mamlaka husika kama vile Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ili hatua zaidi ziwezekuchukuliwa.

Hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kudhibiti kikamilifu vitendo vya rushwa kuelekea uchaguzi mkuu; Waziri Mkuu anasema "Watu wamezoea vitendo vya ruhwa kwenye uchaguzi, serikali tumeagiza kwa kamati za ulinzi na usalama zishirikiane kuhakikisha kwamba hakuna vitendo vya rushwa katika uchaguzi na yeyote ambaye anajihusisha na rushwa asiachwe."

Vilevile Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa, anawataka makamanda wa Takukuru katika wilaya zote nchini wahakikishe wanawakamata wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa wakiwamo na wapambe ambao wanachochea vitendo vya rushwa. Ili kupata maendeleo ya watu ni lazima wapatikane viongozi wa watu kwa ajili ya kuwatumikia wapigakura.

Kiongozi anayeingia madarakani kwa rushwa atajikita katika kuhakikisha anarejesha fedha na mali zake alizotumia kupata uongozi.

Halikadhalika, wananchi walionunulika kwa rushwa wanakosa ujasiri wa kumwajibisha kiongozi wao kwani wao ni sehemu ya uongozi mbaya uliopo kwa kukubali kupokea rushwa na kuuza haki yao ya kuchagua kiongozi bora.

Wapo wagombea bora na wenye uwezo katika vyama vya siasa ambao wanamudu kuwatumikia wananchi ambao hawapo tayari kununua uongozi kwa kutoa rushwa ili wachaguliwe; hao ndiyo wagombea ambao wapigakura wanapaswa kuwachagua kwani watawajibika moja kwa moja kwa wananchi waliowachagua.

Pamoja na wajibu walionao Takukuru kushughulikia vitendo vya rushwa katika uchaguzi, wananchi tuwe sehemu ya kuwasaidia Takukuru kwa kuwapa taarifa za vitendo vya rushwa.

Taasisi hii inao wajibu wa kutunza siri ya raia wema watakayeisaidia kuwapatia taarifa kwa kuripoti vitendo vya rushwa katika uchaguzi. Uchaguzi mkuu Tanzania wa mwaka 2020 bila rushwa inawezekana.

Viongozi bora watapatikana bila rushwa. Tafakari mwananchi, chukua hatua.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0765-409249.***

> Kwa muktadha wa uchaguzi, mtoa chai au takrima huwa ni mgombea wa nafasi ya uongozi au wapambe wa mgombea na mpokeaji huwa ni mwananchi au mpigakura.




Wadau wakihamasisha kwa mabango kupiga vita rushwa. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

# Ni wakati wa kufundishana kukataa 'chai' ya uchaguzi



Fikra za mwaka wa uchaguzi kuwa ndiyo msimu wa utajiri huchangia vitendo vya rushwa. **PICHA: MTANDAO**

SUALA la viongozi wengi wa kisiasa na sekta nzima ya siasa kuonekana kama matunda ya rushwa kunakilazimisha Chama Cha Mapinduzi na serikali ya awamu ya tano, kupambana na kuong'oa shina la saratani ya ufisadi kwenye uchaguzi ambako ndiko kulikokuwa na mizizi ya janga hilo.

Ni ukweli kuwa madiwani, wabunge wa majimbo, viti maalumu na hata wajumbe wengine wa ngazi mbalimbali za kisiasa kwenye vyama walikuwa wanahusishwa na madai kuwa ni matunda ya rushwa ni kwa sababu wanapatikana kwa kutoa fedha na mali ili kununua wajumbe wanaohusika na kuchuja, uteuzi wa wagombea lakini pia na wapigakura ili wawachague.

Rushwa ya ngono nayo kwa kinamama ilichafua uwanja wa siasa. Wanadaiwa walikuwa wanatoa miili kwa wanaohusika na kupendekeza na kuteua wagombea wa viti maalumu na hata kwenye majimbo.

Jambo hili lilisababisha uongozi wa vyama, mihimili mingine ya dola kuchafuka kwa ufisadi kwa kuwa kilichozaliwa kwa njia haramu nacho bila shaka ni haramu na ndivyo hali ilivyokuwa.

Rushwa iliota mizizi ikianzia vijijini kwa kuchafua na kuharibu maadili ya viongozi, kuliingiza taifa kwenye tamaa za viongozi na wananchi kuchukua chao mapema.

Janga hilo lilipelekea na kusababisha hasara kuanzia wizi ya fedha za maendeleo, ubadhirifu kwenye manunuzi ya umma, mikataba ya kilaghai ya kiuwekezaji, kandarasi za ndani na za kimataifa na kusababisha taifa kuzidi kudidimia kwenye umaskini wakati kundi la watumishi wa uma walio katika mihimili ya dola wakineemeka na kutajirika kwa njia haramu.

Ni vyema CCM ilivyotangaza kuwa hakuna mgombea atakayepenya kwa kutoa rushwa ili kununua wajumbe na wapigakura.

### YUPI KIONGOZI BORA

Lakini, pamoja na jitihada za CCM ni vyema pia mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa (Takukuru) kuwapa elimu ya uraia wananchi na wapigakura kujua na kutambua sifa za viongozi bora.

Kiongozi bora anatakiwa kuwa na sifa gani? Kiongozi huyo si yule waliyemzoea akiwapa chai -kanga, madera, fulana, sukari, chakula kama pilau, pombe na mchele wa kupikwa nyumbani. Takukuru na asasi za kiraia watoe maelezo. Ni yupi ambaye ni kiongozi bora.

Ni wakati wa umma kujua ni sifa zipi zinamwendea kiongozi mweledi na watumie njia gani kumpima na kumpata wakati huu wa kueelekea uchaguzi mkuu.

Ni vyema pia kuwa na mfumo wa kudhibiti nidhamu za viongozi wa kisiasa kwa kuhakikisha kuwa jamii inatoa taarifa za kupokea zawadi na vitu kutoka kwa anayetaka kuwa mbunge, diwani au hata kama yuko madarakani.

### KUWEKA MALENGO

Mbunge au diwani atakapoingia kwenye kuchaguliwa au kwenye uongozi anatakiwa kuweka malengo bayana ya mambo ambayo kama kiongozi anayasimamia utekelezaji wake.

> Madaraka na malipo ya ziada wanayopata wanasiasa wanastahili? Au kuna watu wengine wangefanya majukumu hayo hivyo kutoa fursa za ajira na kipato wa raia au wapigakura wao?

Aseme atafanya nini kwenye usafiri, miundombinu, maji, elimu na siyo kuwaletea wapigakura sukari, kanga na kuwanyesha pombe. Atoe ahadi zake kwa maandishi na kuahidi kile atakachofanya kwa miaka mitano na aonekane akitimiza ahadi hiyo.

Kwa mfano, azungumzie ujenzi wa madarasa na kusomba mawe kujenga daraja au soko na atofautishe na zile zitakazofanywa na halmashauri au serikali kuu.

Akishindwa wananchi wawe na haki ya kusitisha mkataba wake wa kuwaongoza na kumweleza kuwa hawajibika kwa ahadi zake.

Pendekezo hili liliwekwa kwenye rasimu ya katiba mpya iliyolenga kuwapa nguvu wapigakura kumng'oa kiongozi wao wa kisiasa na kudhibiti kukosekana uwajibikaji. CCM imeshaonyesha njia ya kuondoa au kupunguza msukumo wagombea uongozi kutoa mlungula kwa wapiga kura kwa hiyo wapigakura inawapasa kukwepa rushwa.

Chama nacho kichunguze na kubainisha ni jambo au mambo gani yanawasukuma viongozi kutoa 'chai' ili wafanikiwe kushinda uchaguzi?

Kwa hali ya kawaida ambayo Watanzania walivyozoea kwa miongo mingi kabla na baada ya kupata uhuru ni uongozi ni dhamana.

Kwa hiyo ilichukuliwa kuwa ndivyo katika nchi nyingi, raia 'hujitolea na kujitoa mhanga' kugombea uongozi ili kuitoa jamii kutoka kwenye hali ya chini na kuwapeleka hali ya juu au bora.

Na kuna baadhi ya watu hujitokeza kwa ajili tu ya kusaidia nchi ifanikishe malengo yake kimaendeleo bila kujali hata kama wataitwa wapenda sifa/

Mfano wa kiongozi huyo ni Vladimir Putin', Rais huyu wa Russia angeweza kuitwa "ego"au "self-esteem", ambaye amekuwa tayari kuchukua nafasi ya uongozi bila malipo yoyote ya ziada ili kuifikisha Russia kwenye kiwango anachokitamani ifikie.

Kutokana na rushwa dhana ya uongozi wa aina hizi unapotea. Katika nchi nyingi za Kiafrika watu huamua kugombea madaraka kwa madhumuni makubwa ya kufanikisha njaa zao.

Kwanza kujipatia pesa kutokana na mshahara mnono na marupurupu ya uongozi. Pia kutumia vyeo kama nyezo ya kufanikisha biashara au uwekezaji binafsi. Wengine wanategemea kutumia vyeo watakavyopata baada ya kuwa viongozi kushawishi biashara zao ikibidi kwa kukwepa kodi, kufanikiwa kupata zabuni mbali mbali au hata kukwepa kodi na kutumia cheo kama kinga dhidi ya ufisadi.

Yote anayafanya hata kabla ya kuwa kiongozi na apofikia kwenye uongozi anatimiza azma

Rushwa imesababisha watu au wahalifu ambao wanapoona wanatuhumiwa kwa jambo baya kama mauaji, ufisadi na tuhuma nzito kukimbilia kugombea uongozi wakitegemea kuwa wakishapata cheo, vyombo vya sheria vitawaogopa.

Wapo waliofanikiwa zama hizo na kujichanganya na wadau wakijiita wafadhili wa mambo mbalimbali ili kujificha na kujisafisha.

### KUHUSU MARUPURUPU

Uongozi wa Tanzania umeondoa pazia hilo la kujinufaisha kama ulifanya ufisadi unashughulikiwa na umeanzisha mahakama ya wahujumu uchumi na ufisadi.

Hii ina maana kuwa pamoja na jitihada hizo serikali ni lazima iangalie kwa jicho la tatu hatua ya kupunguza nguvu ya kutamani mshahara na marupurupu manono ya wanasisa ukilinganisha na kazi nyingine.

Madaraka na malipo ya ziada wanayopata wanasiasa wanastahili? Au kuna watu wengine wangefanya majukumu hayo hivyo kutoa fursa za ajira na kipato wa raia au wapigakura wao?

Lakini pia, kuangalia upya ni watu wenye sifa gani wanastahili kupewa dhamana ya uongozi? Wakishapewa je, tabia zao ni kutumia madaraka kujilimbilikizia mali au kutekeleza majukumu ambayo wananchi waliwatuma?

Ili kumaliza rushwa ufumbuzi wa kudumu unaweza kuwa kuimarisha mifumo ya kuwachuja wagombea uongozi ambayo inatumiwa na vyama vya siasa, hili CCM imeanza kulifanya.

Aidha, kusimamia utii wa kanuni za maadili ya viongozi wa umma na kuzuia rushwa. Kuweka mkazo kwenye usimamizi wa maadili yanayosimamiwa na vyombo kama Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Lakini, hata kwa kutumia mifano hii inabainika kuwa mifumo na taasisi pekee yake haitoshi. Lazima viendane na 'utashi wa kisiasa' wa kuhakikisha sheria na taratibu zilizowekwa zinaheshimika.

Mifano ya kuhimiza uwajibikaji na uadilifu kama Rais John Magufuli, alivyoonyesha baada ya kuanza kuongoza awamu ya tano, aidha, maelekezo ya kupitisha majina ya wagombea yanayotangazwa na kusimamiwa kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu.



# OSHA yasisitiza usalama mahala pa kazi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahala pa kazi nchini (OSHA,) umezitaka sekta mbalimbali zilizopo chini ya sheria za usalama kazini, kuzitii na kuzifuatia, ili kuepukana na adhabu zake.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkaguzi Mwandimizi wa Mazingira sehemu za kazi Kanda ya Kati, Venance Buliga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa ofisini kwake kuhusu ukiukwaji wa sheria, unaofanywa na sekta mbalimbali hapa nchini.

Alisema serikali iliona vyema katika kupambana na ajali mbalimbali, maeneo ya kazi kwa kuweka sheria ya usalama mahala pa kazi ili kuepukana na ajali zinazoweza kutokea kwenye maeneo mbalimbali.

"Pamoja na kuwapo kwa sheria hiyo na taratibu zake katika maeneo ya kazi, OSHA imebaini kuwa ajali zinazotokea ni uzembe unaosabishwa na wamiliki wa sehemu hizo, na usimamizi wake kuwa duni," alisema Buliga.

Alitaja baadhi ya maeneo hayo kuwa ni pamoja na vituo vya mafuta, hoteli na sekta ya ujenzi katika majengo makubwa kuanzia ghorofa tatu na kuendelea, zinatakiwa kuwa na usimamizi mkubwa.

Alisema, kutokana na kutozingatia sheria, imeanza kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika maeneo hayo na wanaobainika kuwa na makosa wanachukulia hatua kali za kisheria pamoja na kutozwa faini.

**"Pamoja na kuwapo kwa sheria hiyo na taratibu zake katika maeneo ya kazi, OSHA imebaini kuwa ajali zinazotokea ni uzembe unaosabishwa na wamiliki wa sehemu hizo, na usimamizi wake kuwa duni," alisema Buliga.**

# Viongozi kisiasa waaswa kufanya siasa kistaarabu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

VIONGOZI wa vyama vya siasa nchini, wametakiwa kuendesha siasa za kistaarabu zinazowaunganisha Watanzania na sio kuwatenganisha katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Pia, vimetakiwa kuimarisha mifumo yao ya ndani ya kuwapata viongozi kwa kuzingatia misingi ya Katiba zao na maadili.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda, alipokuwa akifungua mkutano wa majadiliano ya asasi za kiraia na viongozi wa serikali wa kujadili mkakati wa kuwa na uchaguzi jumuishi na wenye ushirikishwaji wa makundi mbalimbali.

Alisema viongozi hao wapatikane kwa njia ya kidemokrasia kwa kuzingatia usawa wa makundi yote ya kijamii kwa kuzingatia misingi ya Katiba zao na Katiba ya Nchi na miongozo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Niwaombe viongozi wa vyama vya siasa waonyeshe mfano wa kuendesha siasa za kistaarabu, zenye mlengo wa kuwaunganisha Watanzania na sio kuwatenganisha, hatuna taifa jingine la kwenda isipokuwa mama yetu Tanzania, hakuna kiongozi aliyewahi kupata sifa nzuri kwa kuwa chanzo cha mafarakano ndani ya jamii,"alisema.

Alivitaka vyama hivyo kuangalia mifumo ambayo itasaidia kama taifa kutomuacha yeyote nje ya mfumo wowote ikiwamo mifumo ya elimu, uongozi na ufanyaji uamuzi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika linalojishughulisha na masuala ya wanawake (WOWAP), Fatma Toufiq, alisema wadau hao wanaangalia makundi mbalimbali ikiwamo wazee, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kushiriki uchaguzi ili kero zao zisikike katika ngazi mbalimbali za uamuzi.

"Tunaona kabisa kundi la wenye ulemavu bado linahitaji msukumo, kwanza jamii bado haijaona kwamba wenye ulemavu nao sauti yao inapaswa kusikika," alisema.

Naye, Mwakilishi wa Kituo cha Amani, Haki na Msaada wa Kisheria, Catherine Fredrick, alisema anatamani makundi hayo yashiriki uchaguzi wa mwaka huu vizuri kwa wingi bila kuathiri wao kwa namna yoyote.



Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Vumilia Nyamoga (aliyevaa miwani), akipokea sehemu ya msaada wa vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona vyenye thamani ya Sh. Milioni 7.4 kutoka kwa Mwakilishi wa Watanzania wanaoishi nchini Marekani, Kapteni Amos Lwiza (kushoto), katika hafla iliyofanyika katika kituo cha afya Chamwino Ikulu, mwishoni mwa wiki. **PICHA PAUL MABEJA**

# Wajasiriamali watakiwa kufuata utaratibu

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAJASIRIAMALI katika Jiji la Dodoma, wametakiwa kufanya biashara zao kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa ili kujiepusha na migogoro isiyo ya lazima.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akizungumza na waumini wa kanisa la Internation Evangelism Sinai, Ipagala-Dodoma akiwahamasisha kutumia fursa ya uwapo wa Makao Makuu Dodoma.

Alisema pamoja na kuchangamkia fursa ya uwapo wa Makao Makuu Dodoma wahakikishe wanaheshimu maeneo yaliyotengwa ambayo yasiyo rasmi kufanya biashara.

"Najua kuna waumini ambao ni wajasiriamali mjiepushe na migogoro isiyo lazima kwa kufanya biashara maeneo yasiyo rasmi, pamoja na kuwa serikali imetoa uhuru na fursa kwa kila Mtanzania kufanya kazi itakayomletea kipato," alisema.

Aliwahamasisha kujitokeze kuomba maeneo ya kufanya shughuli za ujasiriamali kwa mujibu na utaratibu wa Jiji, badala ya kupanga biashara zao sehemu ambazo ni hatarishi kwao na wateja wanaowahudumia.

Katika hatua nyingine, aliwaomba waumini kuiombea serikali na uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Mchungaji kiongozi wa kanisa hilo, mji mdogo wa Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa, Joshua Ngilodit, aliwataka waumini ndani ya makanisa kufanya shughuli za maendeleo ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema wakati wa kuwategemea wafadhili umeshapitwa na wakati hivyo waumini wanatakiwa kuhakikisha wanajishughulisha kwa kufanya kazi huku wakimtegemea Mungu ili waweze kujiinua kiuchumi na kiroho pia.

Naye Askofu wa kanisa hilo mkoani Dodoma, Silyvester Thadey, alisema uwapo wa makao makuu ya serikali Dodoma ni fursa tosha ya kuondokana na hali ngumu ya maisha kutokana na shughuli mbalimbali zilizopo hivi sasa.

Alisema serikali tangu itangaze kuhamia Dodoma zipo fursa nyingi na kuwataka kuchangamkia kwa kufanya kazi kwa ufanisi zitakazowaletea kipato ikiwamo za ufugaji na kilimo.





## Wataka w'biashara Kiwira kuondolewa maeneo ya hifadhi

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

WAFANYABIASHARA wa ndizi katika soko la Kiwira lililopo Tandale katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, wameiomba serikali kuwaondoa wafanyabiashara wenzao wanaouza kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara wakidai kuwa wanawazibia wateja.

Wanadai kuwa baada ya soko hilo kuanzishwa, serikali iliwaondoa kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara walimokuwa wanafanyia biashara na kuwapeleka katika eneo hilo, lakini baadhi wameendelea kubaki katika maeneo hayo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, James Mwakanyamale, alisema wao waliondolewa na serikali na wakala wa barabara nchini Tanroads wakaweka mabango ya kuwazuia kufanya shughuli zozote ndani ya hifadhi za barabara lakini wenzao bado wapo.

Alisema kitendo hicho kinawafanya wateja waishie barabarani badala ya kwenda kwenye soko ambako wao walihamishiwa na kuhakikishiwa kuwa wateja watakuwa wanaenda huko.

"Tuliambiwa tunahatarisha maisha yetu kwenye hifadhi ya barabara na ndio maana wakatuleta huku, sasa tunashangaa kwa nini wenzetu wanaendelea kuuzia hasa pale Kiwira," alisema Mwakanyamale.

Naye Neema Mwaipopo, alisema kuna baadhi ya maofisa wa serikali wanaendelea kukusanya ushuru hata kwa wale wanaouzia kwenye hifadhi ya barabara badala ya kuwaondoa.

Alimwomba Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Chalya, kuingilia kati kwa maelezo kuwa biashara hiyo inasababisha migogoro baina yao na kwamba hata wao wanatamani kurudi kwenye maeneo yao ya awali ambayo waliondolewa.

"Hata sisi tunatamani kurudi na endapo serikali itaendelea kuwaacha walioko barabarani, hata sisi wenyewe tunaanza kurudi kidogo kidogo na hautakuwa utaratibu mzuri, tunamwomba Mkuu wa Wilaya atusaidie," alisema Neema.

Katika maeneo yote ya barabara ambayo serikali iliwaondoa wafanyabiashara, Tanroads waliweka mabango ambayo yanawazuia wananchi kuendelea kufanya biashara kwenye maeneo hayo lakini kwenye baadhi ya maeneo bado wafanyabiashara wanaendelea kuuzia.

# Wadau wa kilimo wakerwa utitiri wa taasisi zinazokusanya kodi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WADAU wa kilimo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wamelalamikia wingi wa taasisi zinazokusanya kodi kwenye biashara ya pembejeo hasa viuatilifu wakidai kuwa zinasababisha uwepo wa kodi nyingi ambazo ni kero kwa wananchi.

Wakizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo maalum ya udhibiti endelevu wa visumbufu vya mazao yaliyofanyika kwa wiki moja jijini Mbeya, wadau hao ambao ni wakulima, wauzaji wa viuatilifu, maofisa ughani na wengine, walisema kuna taasisi nyingi za serikali ambazo zimekuwa zikipita kukusanya kodi na ushuru kutoka kwenye biashara ya pembejeo na kusababisha usumbufu.

Kostalia Kiduko, alisema tozo hizo kutoka kwa taasisi tofauti za serikali pia zinasababisha pembejeo kuuzwa kwa bei ya juu na kuwa mzigo kwa wakulima hasa maskini ambao uwezo wao wa kununua pembejeo ni mdogo.

"Taasisi zinazokusanya kodi kutoka kwa wauzaji wa pembejeo ni nyingi mno na kwa kweli zimekuwa kero maana utakuta leo wanakuja TPRI, kesho OSHA, siku inayofuata wanakuja Zimamoto na baada ya siku mbili wanafika TRA na kila taasisi inahitaji fedha, hapa lazima bei ya pembejeo iwe juu," alisema Kiduko.

Kiduko aliishauri serikali kuunganisha taasisi hizo ili kubakia na taasisi moja ambayo itakusanya ushuru na kodi ya serikali kwa tija bila kusababisha usumbufu kwa wauzaji wala kuwaongezea wakulima mzigo. Mfanyabiashara mwingine wa pembejeo, Julius Mwakitalu, alisema kuwa uwepo wa taasisi nyingi za serikali ambazo kila moja inakusanya kodi na ushuru kwenye pembejeo unasababisha kuwapo kwa mianya ya rushwa na kupunguza ufanisi na mapato ya serikali.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Nchini (TPRI), Dk. Margareth Mollel, alikiri kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu uwapo wa kodi nyingi kwenye biashara ya viuatilifu, lakini akasema suala hilo lipo nje ya uwezo wake.

Molell alisema suala hilo ni la kisera, na kwamba taasisi zote zinazolalamikiwa zimeundwa kisheria hivyo hawezi kuzizungumzia wala kuwaahidi wadau hao kutatua tatizo hilo.

Badala yake alisema kuwa suala hilo amelichukua na atalifikisha kwa waziri mwenye dhamana ambaye ndiye anaweza kulishughulikia na kutoa ufumbuzi wa tatizo hilo.

"Hapa mimi nashughulikia masuala ya TPRI, sina uwezo wa kuwazuia TRA kuja kukusanya kodi wala OSHA kufika kwenye maeneo yenu ya kazi, hii ni kwasababu taasisi hizi zipo kwa mujibu wa sheria, lakini suala hili nalichukua nitalifikisha kwa waziri ili aweze kuchukua hatua ya kumaliza malalamiko yenu," alisema Mollel.

Wakizungumzia mafunzo hayo, waratibu wa mafunzo hayo ambao ni maofisa kutoka TPRI, waliwataka wadau hao kuzingatia maelekezo ambayo wameyapata ili kuepusha madhara yatokanayo na viuatilifu.



Baadhi ya vijana wakiuza mafuta ya petroli kwenye chupa katika Mji wa Mlowo, wilayani Mbozi, mkoa wa Songwe jana, kutokana na uhaba wa bidhaa hiyo, kwenye vituo vya kuuzia mkoani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waomba serikali iwaunge mkono ujenzi kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WANANCHI wa Kata ya Ilungu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kuwasaidia kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha kata hiyo kilichopo katika Kijiji cha Ifupa wakidai wameishiwa nguvu.

Walitoa ombi hilo juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa anazindua kituo hicho ambacho wamekijenga wenyewe kwa kuchangishana fedha na baadhi ya wadau akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Makampuni ya IPP, marehemu Dk. Reginald Mengi, ambaye aliwachangia Sh. milioni 25.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Kituo hicho, Zacharia Noti, alisema wananchi wa Kijiji cha Ifupa walianza kuhamasishana kujenga kituo hicho mwaka 2017 baada ya kuona wanapata tabu ya kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya.

Alisema walikuwa wanasafiri umbali wa zaidi ya kilomita 70 kwenda katika hospitali mbalimbali zilizopo katika Jiji la Mbeya ama kwenda katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi, na kwamba gharama za usafiri zilikuwa kubwa na zilikuwa zinawatesa.

Alisema licha ya kwamba huduma za matibabu zilikuwa zinapatikana mbali, lakini hata hali ya usafiri ilikuwa ngumu kwa maelezo kuwa barabara za eneo hilo ni mbaya hasa kipindi cha masika ambapo zinakuwa na maji mengi.

"Tulianza kufanya harambee kila siku ya Ijumaa na tumepambana sana mpaka hapa tulipofikia, hawa wananchi wamefikia hatua wamechoka sana hivyo tunaiomba Serikali ituunge mkono kama ambavyo inafanya katika maeneo mengine," alisema Noti.

Alisema pamoja na kwamba ni Kituo cha Afya cha Kata, lakini kimejengwa na kijiji kimoja cha Ifupa pekee kwa maelezo kuwa awali baadhi ya wanasiasa waliingiza siasa kwenye mradi huo na kusababisha baadhi ya vijiji kushiriki.

Noti aliishukuru Serikali ya Wilaya ya Mbeya kwa ushirikiano ambao iliwapatia kwa maelezo kuwa iliwapelekea ramani na michoro pamoja na wataalamu wa kushirikiana nao kwenye ujenzi.

Naye Tumaini Mkoma, alisema wanawake walikuwa ndio waathirika wakubwa wa tatizo la upatikanaji wa huduma za afya mbali na eneo lao.


Alisema mpaka wananchi wa kijiji hicho walifanya harambee 89 ambazo ziliwawezesha kukamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), nyumba ya kuishi watumishi wawili pamoja na jengo la mama na mtoto ambalo limefikia hatua ya uwezekaji.

"Tulikuwa tunatumia zaidi ya saa saba kwenda kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, muda huo ni mrefu sana na ilikuwa inahatarisha maisha yetu hasa wanawake, tumekuwa tukiona serikali ikifanya mambo makubwa hivyo nasi tunaomba itushike mkono," alisema Tumaini.

Chalamila aliwapongeza wananchi hao kwa mwamko walioounyesha kwenye ujenzi wa kituo hicho na akaahidi kuwasaidia kuwaomba wadau wachangie ujenzi wa miundombinu iliyobaki.

Aliwachangia Sh. 1,000,000 na akaendesha harambee ambayo ilisaidia kupatikana Sh. milioni 3.2, huku aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, akiahidi kuwachangia mifuko 200 ya saruji.

Aliwataka wananchi wa maeneo mengine kuiga mfano wa wananchi wa Kijiji cha Ifupa kujitolea kuchangia miradi ya maendeleo ambayo ni kwa ajili ya manufaa yao wenyewe.



# ZEC: Hatujatangaza tarehe ya uchaguzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, amesema tarehe ya kufanyika Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar haijafahamika.

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema anashangaa kusikia baadhi ya watu wakisema kuwa uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ni Oktoba, mwaka huu.

"Bado sisi Tume ya Uchaguzi hatujatoa tarehe ya mwezi wa kufanyika uchaguzi mkuu kwa sababu bado hata Baraza la Wawakilishi halijavunjwa,"alisema.

Alisema wakati utakapofika ZEC itatangaza tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ili wananchi waweze kuwachagua viongozi wanaowataka.

Naye Mkurugenzi wa Tume, Idarous Faina, alisema kuwa Tume hiyo imeshamaliza kazi ya uhakiki wa daftari la kudumu la wapiga kura na inatarajia kuanza vitambulisho vya kupiga kura hivyo wananchi wasubiri kutangazwa utaratibu wa utoaji wa vitambulisho hivyo. Alisema Tume hiyo pia itachakata taarifa za daftari ili kubaini walioiandikisha mara mbili.

Katika hatua nyingine wajumbe wa kamati ya maadili ya uchaguzi wamesema ukweli, uwazi na uwajibikiaji baina ya Tume ya Uchaguzi, Jeshi la Polisi na vyama vya siasa ndio moja ya mafanikio ambayo yataleta mabadiliko zaidi katika uchaguzi mkuu.

Wakizungumza katika mkutano wa kamati hiyo wa kuipitia rasimu ya kanuni za maadili ya uchaguzi, walisema kila mmoja atalazimika kufuata na kuzingatia kanuni za maadili katika kipindi chote cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Walisema licha ya kuwapo mafanikio makubwa baina ya Tume ya Uchaguzi na wadau wake, lakini ina wajibu wa kuipa nguvu zaidI kamati hiyo ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kufikisha ujumbe wa maadili hayo kwa wahusika wa masuala ya uchaguzi.

Mwenyekiti wa kamati ya maadili ambaye ni mjumbe wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Khamis Ramadhan Abdalla, alisema lengo la kuunda kamati hiyo ni kuona uchaguzi mkuu unafanyika kwa kufuata miongozo ya maadili katika hatua zote muhimu ikiwamo kampeni za uchaguzi za wagombea wote kwa ngazi ya uraisi, wajumbe wa baraza la wawakilishi na madiwani.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Hamid Mahmoud, aliwahakikishia wajumbe wa kamati kuwa Tume itaendelea kusimamia maadili na kuhakikisha uchaguzi mkuu unafanyika katika hali ya uhuru na uwazi.

## Katibu Mkuu Demokrasia Makini ajitosa urais

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha Demokrasia Makini jana kimefungua milango ya kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar baada ya Katibu Mkuu wa chama hicho, Ameir Hassani Ameir, kuchukua fomu hiyo na kuahidi endapo atachaguliwa ataboresha sekta ya elimu na afya visiwani hapa.

Ameir ameahidi kuleta mageuzi katika sekta ya Sayansi na Teknolojia visiwani hapa endapo Chama cha Demokrasia Makini kitamteua kuwa mgombea wa nafasi ya urais na kupata ridhaa ya Wazanzibari.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea fomu, Ameir alisema ataboresha kwa kasi sekta ya elimu nchini ambayo haijafikiwa ipasavyo.

"Vipaumbele vyangu ni vingi sana, lakini endapo ntachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar naahidi kuboresha elimu hasa Sayansi na tekhnolojia pamoja na afya bure kwa Wanzanzibari wote," alisema Ameir.

Pia, alisema atadumisha huduma zote muhimu kwa wananchi kama majisafi na salama na kwamba huduma zote zitakuwa ni bure.

Alisema, atahakikisha anakuza utalii wa Zanzibar wenye tija kwa wananchi wote kwa kuzalisha ajira nyingi kwa vijana na kukuza pato la taifa na pato la mtu mmoja mmoja kupitia sekta hiyo.

"Endapo nitachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar huduma muhimu kama vile majisafi na salama itakuwa bure, lakini ntahakikisha utalii uliokuwa katika visiwa hivi unawanufaisha Wanzanzibari wenyewe kwa kuzalisha ajira nyingi sana," alisema.

Kadhalika, atahakikisha Zanzibar inajengeka kimiundombinu kuwa mizuri na kuhamasisha kujengwa kwa viwanda vikubwa na vidogo ili kuongeza uzalishaji pamoja na ajira kwa vijana visiwani humo.

Alisema visiwa vya Zanzibar vina rasilimali za kutosha pamoja na fursa mbalimbali na kuahidi endapo atachaguliwa atahakikisha rasilimali zilizopo zinawanufaisha Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Naye Katibu wa Oganaizesheni ya chama cha Demokrasia Makini, John Fulgence Mrere, akimkabidhi fomu kwa mgombea huyo, alisema zoezi hilo tayari limeshafunguliwa rasmi tangu Julai mosi hadi Julai 15 na kuwakaribisha wanachama wengine wajitokeze kuomba kugombea nafasi mbalimbali kama vile ubunge, uwakilishi, udiwani pamoja na urais wa Zanzibar na urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wenye uwezo.

Katibu Mrere alisema fomu kwa nafasi ya urais ni Sh. 300,000, ubunge na uwakilishi Sh. 50,000 na udiwani Sh. 10,000.



Mkurugenzi, Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar, Daima Muhamed Mkalimoto, akifungua mafunzo ya wasaidizi wa sheria yaliyofanyika Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Migogoro ya ndoa inavyochangia utelekezaji watoto

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MIGOGORO ya ndoa kwa wanandoa Zanzibar imekuwa ikiongezeka hali inayosababisha baadhi ya wanawake na watoto kutelekezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya mkutano wa kuwajengea uwezo wasaidizi wa sheria Zanzibar, Msaidizi wa Sheria Wilaya ya Magharib B Unguja, Asia Juma Suleiman, alisema wanapokea migogoro mingi ya ndoa ambayo husababishwa na mambo mbalimbali.

Alisema miongoni mwa sababu hizo baadhi ya wanandoa kutokuwa waaminifu katika ndoa zao hali ambayo inasababisha migogoro na wakati mwengine ndoa kuvunjika.

"Wanandoa wengi wamekuwa wakitufuata sisi wasaidizi wa sheria ili kuwasaidia masuala ya sheria baada ya kuwa na migogoro katika ndoa zao," alisema.

Alisema wamegundua pia baadhi ya migogoro hiyo ya wanandoa inasababishwa na baadhi ya wanaume kwa kutoeleza ukweli kwa mweza wake kabla ya kufunga ndoa.

Pia, baadhi ya wanaume wanapoenda kuoa mke mwengine bila kutoa taarifa kwa mke mkubwa na anapogundua ndipo mgogoro unapoanzia.

Msadizi huyo wa sheria alisema elimu ya ndoa bado itahitajika ili kupunguza migogoro ya ndoa.

Alisema mafunzo waliyopatiwa yatawasaidia kufanya kazi zao kwa jamii ikiwamo kusaidia kutatua migogoro hiyo bila ya kuvunja sheria.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya msaada wa kisheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said, alisema wasaidizi wa kisheria walikua hawatambuliki katika jamii na baadhi ya viongozi wa shehia walikuwa hawawapi ushirikiano. Alisema baada ya kuwatambulisha katika jamii hivi, sasa imewatambua na kuwakubali na kupeleka malalamiko yao kwa lengo la kutafutiwa ufumbuzi.

Katika kuelekea uchaguzi mkuu, Mkurugenzi huyo aliwataka wasaidizi wa kisheria kufanya kazi zao bila kuegemea upande wowote wa vyama vya kisiasa ili kufanya kazi kwa ufanisi.

Kwa upande wake Mratibu wa Mradi wa Shirika la Legal Services Facility, Joseph Magazi, alisema shirika hilo limeamua kuwajengea uwezo wasaidizi wa sheria kwa sababu jamii bado inakosa haki zao kutokana na kutojua sheria.

Alisema baadhi ya jamii inakosa haki zao kwa kutojua sheria ikiwamo haki ya mirathi na umiliki wa ardhi.

Akifungua mafunzo hayo ya siku tano kwa wasaidizi wa sheria, Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Daima Muhamed Mkalimoto, aliwataka wasaidizi hao kuyafanyia kazi mafunzo hayo waliyopatiwa ili kuleta maendeleo katika masuala ya msaada wa kisheria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**Anayehitaji kukodi gari Scania** Mende Tipper 8x4 kwa mkataba wa kudumu. Gari itakuwa tayari mwishoni mwa July 2020. Inafaa kwa miradi kama ya ujenzi wa au uchimbaji madini. Mawasiliano 0784-668-810.

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ina ghorofa moja, ina godown ina fremu 10 na ina eneo kubwa wazi, ipo Dar es Salaam. Mawasiliano 0757 079057


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;177/2020**

**Ombi la ZAKAYO MUSSA NYALUSI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu EMILIA WILLIAM NYENYEMBE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/07/2020.

115802102

**TAARIFA YA KUPOTELEWA NA HATI YA NYUMBA - 6 JULY2020**

**Kampuni ya Sea Salt Ltd** yenye ofisi zake Ubungo Business Park–ubungo inatangaza kupotelewa na Hati ya Nyumba (Certificate of Occupancy) NAMBA 17346. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chocote cha Polisi au Apige **Simu namba 022 2401454.** Polisi Taarifa: **DAR/MSI/RB/501965/2020**

115801302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;168/2020**

Ombi la **ALBERT MUSA MGAYA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MUSA MOHAMED MGAYA** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/07/2020.

115801602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;155/2020**

Ombi la **MAHADHI ZUKHERI NG'ANGULI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SABAHA ZUKHERI NG'ANGULI Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 14/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/06/2020.

115802202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;146/2020**

Ombi la **RUKIA SAMA MWANGIA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AZAMA FURUWA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/06/2020.

115808102

**KUPOTEA KWA KADI**

**Grace Jacob Maseta** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T206 CAH** aina ya Suzuki iliyotolewa na Mamlaka ya Tanzania . Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochite cha Polisi. Polisi taarifa : **DAR/KIJ/504900/2020**

115802002


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Kenya yalegeza masharti ya corona

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ametangaza mpango wa kufungua tena shughuli za kawaida nchini humo kwa kulegeza vizuizi vilivyowekwa kukabiliana na virusi vya corona.

Katika hotuba yake kwa taifa, Rais Kenyatta (pichani) alisema jana kuwa, mpango huo utafanywa kwa awamu na utajumuisha kuruhusiwa kuanza tena kwa safari za ndege za kimataifa kuanzia Agosti Mosi pamoja na kuondoa marufuku ya kusafiri ndani ya nchi.

**Hadi jana, Kenya imethibitisha karibu visa 7,900 vya virusi vya corona na vifo 160.**

Uamuzi huo umekuja wakati shinikizo linaongezeka nchini humo la kutaka shughuli za uchumi ziruhusiwe baada ya kudorora miezi minne tangu nchi ilipoweka vizuizi vikali vya kukabiliana na virusi vya corona.

Vizuizi vilivyopo vimeathiri kwa kiwango kikubwa sekta muhimu ikiwamo utalii ambao unaajiri mamilioni ya watu nchini humo na chanzo kikubwa cha fedha za kigeni.



Rais Kenyatta alisema, “Safari za ndege za kimataifa za kuingia na kutoka Kenya zitarejea Agosti Mosi 2020” huku marufuku ya kuingia na kutoka mji mkuu Nairobi, mji wa Pwani wa Mombasa na ule wa Kaskazini Mashariki wa Mandera inaondolewa mara moja kuanzia leo.

Hata hivyo, Rais Kenyatta amerefusha siku 30 zaidi ya amri ya kutotoka nje usiku.

Kiongozi huyo ameonya kuwa hatosita kurejesha vizuizi vilivyopo iwapo hali ya maambukizi ya itakuwa mbaya.

“Katika siku 21 zijazo tutatizama mwenendo wa muingiliano na kusambaa kwa virusi. Ikiwa kuna ishara zozote kuwa hali ya ugonjwa inakuwa mbaya hatutakuwa na uamuzi mwingine isipokuwa kurejesha vizuizi” alisema Rais Kenyatta katika sehemu ya hotuba yake.

Hadi jana, Kenya imethibitisha karibu visa 7,900 vya virusi vya corona na vifo 160.

Mlipuko huo umeutikisa uchumi wa nchi hiyo huku Wizara ya Fedha ikisema janga la corona litasababisha kuanguka kwa ukuaji wa uchumi hadi asilimia 2.5 mwaka huu kutoka ukuaji wa asilimia 5.4 mwaka uliopita. **DW**

## Idadi yapunguzwa kuapishwa Rais Malawi

**LILONGWE,** Malawi

RAIS mpya wa Malawi, Lazarus Chakwera, amefuta sherehe za uhuru zilizopangwa kufanyika nchini humo na kupunguza idadi ya watakaohudhuria kuapishwa kwake kutokana na corona.

Sherehe rasmi ya kuapishwa kwa Rais huyo mpya zilipangwa kufanyika jana katika uwanja mkubwa mjini Lilongwe na zilikuwa zikienda sambamba na maadhimisho hayo ya miaka 56 ya uhuru. Malawi imerekodi visa 1,613 vya maambukizi ya corona na haijaweka vizuizi.

Katika hotuba yake ya Jumapili, Rais Chakwera alisema sherehe ya kuapishwa kwake itafanyika katika kambi ya kijeshi na watu 100 pekee walioalikwa ndio watahudhuria.

Chakwera (pichani chini) alishinda uchaguzi wa Rais uliorudiwa Juni 23, kwa kupata asilimia 58.5 ya kura dhidi ya aliyekuwa Rais Peter Mutharika.

Hatua ya kupunguza sherehe hizo imepunguza furaha ya watu waliotaka kusherehekea ushindi huo wa kihistoria, baada ya mahakama kufutilia matokeo ya uchaguzi wa mwaka uliopita ambapo Mutharika alitangazwa mshindi. **DW**





Mohamed Abdullahi Mohamed ambaye alibadilisha uraia wake Marekani kuwa Rais wa Somalia. **PICHA:MTANDAO**

## Trump aishutumu Somalia hakuna serikali

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, anataka kumtumia mbunge Mmarekani mwenye mizizi yake Somalia, Ilhan Omar, kama ajenda ya kampeni yake ya uchaguzi wa Novemba mbali na taifa lake alilozaliwa.

Katika matamshi aliotoa katika mkutano wa kampeni uliofanyika katika eneo la Tulsa, Oklahoma, alimshambulia mbunge huyo mwenye umri wa miaka 37 akidai kwamba anataka kuleta machafuko ya Somalia nchini Marekani.

“Anataka kuifanya serikali yetu kuwa kama taifa la Somali analotoka. Hakuna serikali, hakuna usalama hakuna polisi, hakuna chochote ni machafuko tu. Na sasa anatufunza jinsi ya kutawala. Hapana asante”.

Omar ambaye aliwasili nchini Marekani akiwa mtoto kama mkimbizi 1995, ni mbunge anayewakilisha eneo la Minnesota, ambalo linashirikisha Minneapolis ambapo Mmarekani mweusi George Floyd aliuawa na polisi mwezi Mei, na hivyo kuwasha moto wa maandamano ya Black Lives Matter. Taifa analotoka Omar ndilo ambalo Rais Trump alichagua kulishambuliwa akiwa Tulsa, pengine ili kuwafanya watu kusahau changamoto zinazomkabili nyumbani.

Akijibu, Omar alisema matamshi yake ni ya ‘kibaguzi’.

Aliongezea kwamba, hasira yake inatokana na kwamba katika kura ya maoni ya hivi karibuni amekuwa nyuma ya mpinzani wake mkuu kutoka chama cha Democrats, Joe Biden, katika jimbo lake ambalo ni nyumbani kwa jamii kubwa ya Wasomali Wamarekani.

Rais Trump alimtaja Omar kama mtu aliyejaa chuki, akionya kwamba atakuwa na jukumu la kuchagiza taifa hilo iwapo Biden ataibuka mshindi.

Hii ni kinyume na kwamba wawili hao wamekuwa na maoni tofauti katika chama cha Democrat, huku Omar akimuunga mkono mpinzani wa Joe Biden, Bernie Sanders kushinda tiketi ya chama cha Democrat. **BBC**

## India ya tatu maambukizi corona

**NEW DELHI,** India

INDIA imetangaza kuwa na takriban ya maambukizi 700,000 ya virusi vya corona na kusababisha kuwa taifa la tatu lililoathiriwa zaidi na janga hilo ulimwenguni.

Idadi hiyo ya waathirika wa corona imefanya taifa hilo kulipita Urusi. Wizara ya Afya ya India, ilisema katika muda wa saa 24 zilizopita, imekuwa na maambukizi mapya 24,000 na hivyo kufanya jumla ya idadi ya walioambukizwa hadi sasa kufikia 697,358.

Marekani na Brazil ndizo zinaongoza kwa idadi ya juu ya maambukizi.

Hata hivyo, haitarajiwi kuwa India itafikia kilele chake baada ya wiki kadhaa japo wataalamu wa afya wametabiri kuwa idadi ya maambukizi ya India itapindukia watu milioni moja mwezi huu.

Watu 19,963 wamefariki nchini India kutokana na virusi hivyo, ikiwa ni idadi ya chini ikilinganishwa na mataifa yaliyoathiriwa kwa kiwango kikubwa.

Miji iliyoathiriwa zaidi nchini India na janga hilo ni New Delhi pamoja na Mumbai, kila mji ukiwa na zaidi ya maambukizi 100,000. **DW**

# MARTINEZ HAONDOKI INTER



**MILAN,** Italia

OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amesisitiza Lautaro Martinez "hajaonyesha ishara ya kutaka kuondoka" huku uvumi ukimhusisha kuwa anawaniwa na Barcelona.

Martinez, raia wa Argentina, ambaye alikosa penalti wakati Inter wakichezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Bologna kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumapili, amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kwenda Camp Nou mwishoni mwa msimu huu 2019-20.

Marotta aliulizwa tena kuhusu uwezekano wa fowadi huyo kuondoka San Siro na akajibu kwamba, Inter wanataka kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Lautaro hajaonyesha nia ya kutaka kuondoka hapa," alisema Marotta akinukuliwa na DAZN. "Kiukweli kabisa, Inter haitaki kuuza mabingwa wake au vipaji vichanga. Kama mchezaji mwenyewe angeomba kuondoka, tungetathmini kwa pamoja, lakini hadi sasa, hakuna ombi kama hilo.

"Naamini kwamba, kuwa mchezaji kijana, inaweza kukufanya uimarike zaidi kiuchezaji kwa muda zaidi hapa Inter.

"Kuwa mchezaji wa Inter inamaana kuwa upo sehemu ya klabu kubwa hivyo, huwezi kuamua tu kuondoka kwani unajisikia fahari kucheza hapa."

# Guardiola: Man City haitasajili wapya

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, haamini kama kipigo walichokipata Jumapili kutoka kwa Southampton kwenye mechi ya Ligi Kuu England, kinawafaya kuwa na uhitaji wa kusajili wachezaji wapya.

Guardiola alishuhudia City wakipata kipigo chao cha tatu cha ugenini katika ligi hiyo msimu huu, baada ya kukubali kufungwa 1-0 na Southampton kwenye dimba la St Mary's.

Baada ya kutoka kuwafunga mabingwa wapya Liverpool 4-0, City, ambao walimpumzisha Kevin De Bruyne na nyota wengine kadhaa, walijikuta wakiangukia pua na sasa wamepitwa pointi 23 wakiwa nafasi ya pili.

Nyota wa Napoli, Kalidou Koulibaly na David Alaba wa Bayern Munich wamekuwa wakitajwa kuwa ni miongoni mwa wachezaji wanaowania kusajiliwa pale City mwishoni mwa msimu huu.

Lakini alipoulizwa kuhusu kipigo hicho na kwamba sasa City wanahitaji kusajili wachezaji wapya, Guardiola aliwaambia waandishi wa habari: "Hapana, sidhani.

"Nafikiri tulicheza vizuri, kiukweli kabisa. Tulicheza kwa kujituma na kutafuta ushindi hadi mwisho wa mchezo. Tulicheza dhidi ya Southampton ambao walikuwa na wachezaji 10 kwenye eneo la penalti. Tulifanya vizuri sana.

"Tutautazama tena mchezo na kwa nafasi tuliyokuwa nayo, tunaweza kufanya zaidi. Ni ngumu kutengeneza nafasi zaidi kama tulizozitengeneza."





# *Solskjaer ampigia debe Greenwood England*

**MANCHESTER,** England

KINDA wa Manchester United, Mason Greenwood yupo tayari kuitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia pale Old Trafford, kwa mujibu wa Kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Greenwood mwenye umri wa miaka 18, alifunga mabao mawili wakati United walipoifunga Bournemouth 5-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa Jumamosi.

Mshambuliaji huyo ambaye analinganishwa na nyota wa zamani wa United, Robin van Persie - amefunga mabao 15 katika mashindano yote msimu huu, yakiwamo nane kwenye Ligi Kuu England.

Solskjaer amemsifia Greenwood na kumpa nafasi ya kuitwa kwenye kikosi cha England kinachonolewa na Gareth Southgate.

"Wakati unapoichezea United, nafikiri huo ni mtihani mzuri wa kujipima upo kwenye kiwango gani," alisema Solskjaer, ambaye ameiongoza United kutofungwa katika mechi 16 mfululizo.

"Kama unaweza kuichezea United, hivyo unaweza kucheza katika timu yoyote na Mason ana ubora ambao sio wachezaji wengi wanao.

"Hivyo, anaweza kuichezea England ya wakubwa au chini ya umri wa miaka 21. Najua anafanya vizuri na hapa amepata nafasi nzuri ya kujiweka sawa."

HABARI MICHEZO

# Wachezaji Inter Milan wamkasirisha Conte

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte ana matumaini wachezaji wake angalau wanahisi kwa "asilimia moja" kuhusu kipigo cha 2-1 kutoka kwa Bologna kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia pale San Siro, Jumapili.

Inter walianza kwa bao la kipindi cha kwanza lililofungwa na Romelu Lukaku kabla ya Bologna kumpoteza mchezaji wake, Roberto Soriano aliyelimwa kadi nyekundu dakika ya 57.

Lautaro Martinez angeweza kuongeza bao, lakini penalti aliyopiga iliokolewa na golikipa, Lukasz Skorupski.

Bologna walirudi mchezoni na kupata mabao mawili ndani ya dakika 16 za mwisho, shukrani kwa mabao ya Musa Juwara na Musa Barrow, huku pia Inter wakimpoteza, Alessandro Bastoni aliyeonyeshwa kadi nyekundu kwa mchezo mbaya.

Conte, ambaye alitumia saa nzima akiwa na wachezaji wake kwenye vyumba vya kubadlishia nguo baada ya mchezo huo kabla ya kuzungumza na waandishi wa habari, hakuficha hisia zake na alisema wachezaji walitakiwa kukasirishwa na matokeo hayo.

"Inakatisha tamaa, hasa kwa upande wangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Natumaini nao wachezaji angalau watakuwa na hisia ya asilimia mia moja kutokana na kipigo hiki.

"Nimekasirika mwenyewe kwa sababu mimi ndio kocha. Ni jukumu langu, kwani mimi ndio ninayewaongoza ni sawa tu kwa upande wangu kuwa na hasira. Halafu wachezaji nao wanatakiwa kujifikiria."





# MANDZUKIC AVUNJA MKATABA QATAR

**DOHA,** Qatar

STRAIKA wa zamani wa Juventus, Mario Mandzukic amevunja mkataba wake na klabu ya Al-Duhail ikiwa ni baada ya miezi sita kupita tangu ajiunge nayo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 34, alihamia katika klabu hiyo ya Qatar Desemba mwaka jana baada ya kutokuwa na nafasi kwenye kikosi cha Maurizio Sarri ambaye anaiongoza Juve.

Lakini straika huyo ambaye alifunga bao la ushindi katika mechi ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Dunia kati ya England na Croatia mwaka juzi, kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa amefikia uamuzi wa kuvunja mkataba baada ya kufikia maelewano na klabu hiyo.

"Ninapenda kuchukua nafasi hii kushukuru ukaribu na ushirikiano niliopata nilipokuwa Qatar na ninaitakia kila na kheri klabu hii na timu katika siku zake zijazo," alisema Mandzukic.

Mandzukic amecheza mechi tano tu za Ligi ya Qatar akiwa na Al-Duhail, lakini hakufanikiwa kufunga bao hata moja kwa kipindi hicho kifupi alichodumu klabuni hapo.

Hata hivyo, straika huyo alifunga bao moja katika mechi ya Ligi ya Mabingwa wa Asia dhidi ya Persepolis iliyochezwa Februari 11, mwaka huu.

Kabla ya kwenda Qatar, Kocha wa Juventus, Sarri alikuwa hamtumii Mandzukic kwenye kikosi chake cha kwanza, huku kukiwa na tetesi za kuhusishwa na Manchester United.

Sasa huenda akarejea Italia, baada ya AC Milan na vinara wa Serie B, Benevento wakitajwa kuwinda saini ya straika huyo mwenye umri wa miaka 34.

# *Klopp azungumzia usajili wa Thiago*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amemtaja, Thiago Alcantara kama "mchezaji mzuri", lakini hakuwa tayari kusema zaidi kuhusu kiungo huyo wa Bayern Munich.

Thiago mwenye umri wa miaka 29, mkataba wake unamalizika mwakani na amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua Anfield.

Alipoulizwa kuhusu uhamisho wa kiungo huyo wa zamani wa Barcelona, Klopp alisifia tu ubora wa Thiago.

"Unaweza kushangaa kama sitakujibu swali hilo? Kwa sababu kamwe huwa sipendi kujibu aina hii ya maswali," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya Liverpool kuibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Aston Villa, Jumapili.

"Thiago Alcantara ni mchezaji mzuri. Nawapenda wachezaji wengine kama yeye, hilo tu ndio ninaloweza kuzungumza kwa sasa."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AJIANDAA KUSTAAFIA BARCA

●●● Bosi wa vigogo hao wa Hispania afunguka baada ya kuwapo kwa tetesi za nahodha huyo...

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amesisitiza Lionel Messi mara zote ameonyesha nia ya kutaka kustaafia soka lake akiwa Camp Nou wakati huu kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa yake.

> **Mkataba wa sasa wa Messi na Barca unamalizika mwakani, lakini taarifa zimekuwa zikivuma kwamba, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or anataka kuondoka mwakani.**

Nahodha huyo alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi Jumapili, wakati Barca wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Villarreal kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Messi amefikisha pasi za mwisho 19 kwenye LaLiga msimu huu, na Bartomeu aliulizwa kuhusu majaliwa ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 mara baada ya mchezo huo kumalizika.

"Siwezi kuelezea kwa kina nini kinatokea kila wiki. Kuna majadiliano na wachezaji wengi," alisema Bartomeu akinukuliwa na Movistar.

"Messi mara zote ameonyesha nia ya kuwa anataka kustaafu soka lake akiwa hapa Barcelona."

Bartomeu pia aliulizwa kuhusu kocha aliyekalia kuti kavu, Quique Setien baada ya Barca kupitwa pointi nne na wapinzani wao Real Madrid, huku zikiwa zimesalia mechi nne msimu huu kumalizika.

Bartomeu alisema: "Najua kuna uvumi. Sio kweli, hizo ni taarifa za kizushi.

"Quique Setien anaaminiwa na kila mtu, wachezaji, bodi na anafanya kazi nzuri.

Taarifa zaidi zinasema Manchester City itajipanga kumsajili mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Argentina, Messi baada ya mkataba wake na Barcelona utakapomalizika katika majira ya joto mwakani kama kocha wake.

Hata hivyo City itafanya mchakato huo kama Kocha, Pep Guardiola atakuwa ameondoka klabuni hapo.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA KUUZA SITA

CHELSEA inaangalia uwezekano wa kuuza wachezaji wake sita ili kupata fedha za kusaidia kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz (21), ambaye Bayer Leverkusen imetangaza thamani yake ni pauni milioni 90. ***(Express)***

### ARSENAL, NAPOLI VITANI

ARSENAL na Napoli zote zimeonyesha nia ya kumsajili winga wa Newcastle United, Mfaransa, Allan Saint-Maximin, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Le10 Sport in French)***

### ARSENAL, LACAZETTE KUTETA

ARSENAL imejiandaa kuanza mazungumzo na mshambuliaji wake Mfaransa, Alexandre Lacazette, ambaye ana umri wa miaka 29, kwa ajili ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo. ***(Mirror)***

### BELLERIN ANUKIA PSG

PARIS St-Germain inajiandaa kufanya mchakato wa kumsajili beki wa kulia wa Timu ya Taifa ya Hispania na Arsenal, Hector Bellerin (25), ambaye anawaniwa na Juventus pamoja na Bayern Munich. ***(Express)***

### THIAGO NJIA PANDA

KIUNGO wa Bayern Munich, Thiago Alcantara (29), amekuwa haelewi hatima ya uhamisho wake wa kujiunga na Ligi Kuu England, huku Liverpool ikionyesha nia ya kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Hispania kwa dau la pauni milioni 32. ***(Mail)***

### ROSE HAKIJAELEWEKA

BEKI wa Timu ya Taifa ya England, Danny Rose (30), anahofia hatima yake ndani ya Tottenham imefikia mwisho na sasa anatakiwa kuongeza nguvu katika klabu yake ya mkopo ya Newcastle United. ***(Mirror)***

### SEVILLA, ATLETICO VITANI

SEVILLA na Atletico Madrid zinajipanga kuchuana kuwania saini ya kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (32), ambaye anajiandaa kuondoka Nou Camp ifikapo majira ya joto. ***(Marca)***

### XAVI AIPOTEZEA BARCA

BARCELONA imeshikwa na kigugumizi kuhusiana na uamuzi wake wa kumwajiri Xavi kama kocha mpya baada ya kiungo huyo kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuifundisha Al-Sadd ya Qatar. ***(Mail)***

### ANCELOTTI: SIUZI MCHEZAJI

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti amesema hana mpango wa kuuza nyota wake, wakati beki Mfaransa, Lucas Digne (26), mshambuliaji Mbrazil, Richarlison (23), na beki raia wa England, Mason Holgate (23), wanahusishwa na mpango wa kuondoka Goodison Park. ***(Talksport)***

### SCHOLES AILAUMU UNITED

MANCHESTER United imefanya kosa kwa kushindwa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland (19), ambaye alijiunga na Borussia Dortmund akitokea Red Bull Salzburg, kiungo wa zamani wa United, Paul Scholes amesema. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## Maafande JKU, Mlandege vitani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU inatarajia kuwakaribisha vinara, Mlandege katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa JKU, Omar Khamis 'Matu', alisema timu yake imejipanga vema kuelekea mchezo huo ambao malengo yao ni kuondoka na pointi tatu muhimu.

Matu alisema anaamini ushindi pekee ndio utawarejesha kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Kocha huyo alisema licha ya kutokuwa na mdhamini, anafahamu ligi hiyo ni ngumu na yenye ushindani kwa sababu timu zote zimepania kusaka ushindi.

"Tumejipanga kushinda michezo yote iliyobaki ili kujiwekea nafasi nzuri ya kuchukua ubingwa wa ligi msimu huu ambao umekumbwa na misukosuko ya maradhi ya corona," Matu alisema.

Alimtaja mchezaji wake atakayekosa mechi hiyo ni Swedi Hussein ambaye aliumia goti na Haji Wahaji ambae ana homa iliyotokana na uchovu wa mchezo uliopita.

Kiongozi huyo amewataka mashabiki wa timu hiyo kufuata agizo la serikali la kutohudhuria viwanjani ili kuepuka vurugu milangoni kama inavyotokea hivi sasa.

JKU ipo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 46 wakati Mlandege wanaongoza wakiwa na pointi 50 huku KMKM yenye alama 49 ikifuatia.

## Zanzibar walilia Daraja la Kwanza

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WADAU wa soka Zanzibar wameiomba serikali kuruhusu kuendelea kwa mechi za Ligi Daraja la Kwanza ili kupata timu zitakazopanda daraja kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2020/21, imeelezwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliruhusu kuendelea kwa Ligi Kuu tu huku ligi nyingine zikisubiri mwongozo mpya wakati huu bado janga la corona haijamalizika nchini.

Katibu wa Kilimani City inayoshiriki Ligi Daraja la Kanda ya Unguja, Abdulrahman Salum, alisema kwa niaba ya wenzake, serikali iangalie tena uamuzi wa kuruhusu ligi nyingine ili kukamilisha msimu huu na hatimaye kupata timu zitakazopanda daraja kwa haki.

Salum alisema Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ilikuwa imebakisha michezo michache na anaamini ikiruhusiwa tena, watatumia wiki mbili kukamilisha msimu huu huku wakiahidi kufuata mwongozo wa Wizara ya Afya kama inavyotekelezwa katika Ligi Kuu Zanzibar.

"Tunajua serikali inafanya hivi kutokana na kuendelea kujikinga na virusi vya corona, hususani katika zile sehemu ambazo mikusanyiko ya watu inakuwapo , tunawaomba pia waruhusu Ligi Daraja la Kwanza ikaendelea na ikasisitiza taratibu zote za kujikinga na corona zikafuatwa," Salum alisema.



Wachezaji wa Boma FC wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Karume, jijini Dar es Salaam ili kujiandaa na mechi za Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara inayoendelea hapa nchini. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# NAMUNGO YAJIPANGA KUITIBULIA MSIMBAZI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo imetamba inaweza kuharibu sherehe ya makabidhiano ya kombe kwa kupata ushindi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaowakutanisha na mabingwa hao kesho kwenye Uwanja wa Majaliwa, Lindi, imefahamika.

**Ofisa Habari wa Namungo FC, Kindamba Namlia, alisema wamejiandaa kuifunga Simba na kuendeleza rekodi safi ya kutofungwa mechi yoyote ile mpaka sasa, wamecheza mechi 17 mfululizo bila kupoteza.**

Namlia alisema wanatarajia kuonyesha soka la kiwango cha juu na kuwataka mashabiki wa Simba wajiandae kuchukua kombe la ubingwa kimya kimya.

"Simba kwa sasa ni kama mtu aliyepata pesa za mafao, lakini hajui jinsi gani ya kuzitumia. Tumejiandaa kutia jongoo na mchanga kwenye pilau lao, wajiandae kuchukua kombe na kuondoka kimya kimya, kwa sababu sisi tunataka kuendeleza rekodi yetu ya kutopoteza mechi yoyote, nadhani hadi ligi itakapokwisha," alisema Kindamba.

Tangu ilipofungwa na Simba mabao 3-2 Januari 29, mwaka huu, Namungo haijapoteza tena mechi yoyote ile mpaka sasa.

Ni mechi ambayo Shirikisho la Soka Nchini (TFF), imeiteua kuwa ndiyo itaikabidhi Simba taji la ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20, mbele ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo, waliotoka sehemu mbalimbali nchini kushuhudia sherehe hizo.

"Niwatahadharishe tu Simba kwa sababu hata ile mechi ya kwanza, ushindi wao waliupata kwa taabu na mizengwe, na walikuwa kwao, sasa wako Ruangwa kwenye Uwanja wa Majaliwa, ni ngumu sana kutoka huku," Namlia alitamba.

Simba haijashinda mechi zake mbili mfululizo za ligi baada ya kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Tanzania Prisons jijini, Mbeya na juzi dhidi ya wenyeji Ndanda FC kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona.

# *Cheka, Phiri kupigana Septemba*



Cosmas Cheka

**Saada Akida**

PAMBANO la kimataifa kati ya bondia mkongwe wa hapa nchini, Cosmas Cheka dhidi ya Hennock Phiri kutoka Malawi sasa litafanyika Septemba 12, mwaka huu imefahamika.

Awali pambano hilo lilipangwa kufanyika Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri, mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili, promota wa pambano hilo, Kaike Siraju, alisema uamuzi wa kulisogeza mbele pambano hilo umesababishwa na Uwanja wa Jamhuri kuwa na majukumu mengine siku hiyo.

Siraju alisema maandalizi ya mtanange huo yako katika hatua za mwisho na mabondia wote wawili wanaendelea vizuri na programu zao za mazoezi.

"Wamiliki wa uwanja watufahamisha kuanzia Agosti 30, ndio uwanja utakuwa wazi, hivyo tukaona pambano letu lipigwe Septemba 12, mwaka huu, hakuna kilichoharibika," alisema Siraju.

Alisema bondia huyo wa Malawi atawasili nchini wiki moja kabla ya pambano hilo la ubingwa wa Afrika ambalo litakuwa ni la raundi 12 la uzani wa light.

"Tayari Cosmas ambaye ni mdogo wake na bondia bingwa wa zamani wa dunia wa WBF, Francis Cheka ameshaingia kambini chini ya kocha wake, Abdallah Salehe (Comando)," alisema Siraju.

Cosmas aliliambia gazeti hili anafanya mazoezi katika kiwango bora na anaamini pambano hilo atashinda mapema kwa kipigo cha Knock Out (KO).

Michezo
Jumanne Julai 7, 2020
Nipashe



Messi ajiandaa kustaafia Barca UKURASA 22



Golikipa wa Manchester City, Ederson (kulia), akipambana kumzuia straika wa Southampton, Che Adams, kufunga bao la pili katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa St Mary's juzi usiku. City ilichapwa bao 1-0.
**PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, NAMUNGO WAKATI UTAONGEA

## Kocha Sven aeleza mechi hiyo itawasafishia njia kuelekea mchezo dhidi ya watani Jumapili...

**Na Somoe Ng'itu**

SAFISHA njia! KOCHA Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema amekiandaa kikosi chake kuondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Majaliwa, Lindi ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuikabili Yanga.

**Mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, Simba watakutana na Yanga katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA, itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.**

Akizungumzia na gazeti hili jana, Sven alisema anataka kuona kikosi chake kinaweka rekodi ya kucheza fainali za Kombe la FA, baada ya kuwatoa wapinzani wao wa jadi, Yanga ambao waliwafunga kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania walipokutana Machi 8, mwaka huu.

Sve alisema kwa sasa akili yao imeelekea katika kuikabili Namungo na wanatarajia kupata pointi tatu ambazo zitaongeza furaha katika sherehe za kukabidhiwa kikombe.

Alisema mchezo wa Jumatano (kesho), ni sehemu mojawapo ya kukijenga kukiimarisha kikosi chake kuelekea 'hesabu' za kuwaharibia wapinzani wao Yanga katika 'mtangange' wa Kombe la FA, hatua ya nusu fainali.

"Tupo hapa (Mtwara), kama sehemu ya maandalizi ya mchezo wetu ujao dhidi ya Namungo, ikiwa pia ni maandalizi ya mchezo wa FA dhidi ya Yanga, hakuna mchezo mwepesi, wao wanahitaji matokeo na sisi pia tunahitaji matokeo mazuri, tupo kwa ajili ya kupambana na kupata matokeo mazuri na kuvuka hata ya nusu fainali, "Sven alisema.

Naye nahodha wa timu hiyo, John Bocco, alisema wako tayari na imara kuwakabili Namungo ambayo inaundwa na wachezaji wenye uzoefu na ligi hiyo.

Bocco alisema anaimani hawatawaangusha mashabiki wao ingawa wanajua wapinzani wao wana timu nzuri na yenye rekodi nzuri ikiwa nyumbani.

"Sisi kama wachezaji tupo vizuri, tutapambana tupate matokeo, tunajua Yanga ni timu nzuri, na hata Namungo, tulicheza nao mara ya kwanza tulipata matokeo, lakini haikuwa rahisi hivyo, tunajua nao wamejipanga lakini nasi tunataka tuchukue kombe huku tukiwa tumeshinda, " Alisema Bocco.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi cha timu hiyo kitaondoka Mtwara leo jioni na kuelekea Lindi tayari kwa mechi hiyo.

Rweyemamu alisema anawaomba mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi kwa sababu wanataka kukabidhi kombe la ubingwa wakiwa na furaha.

Alisema pia wanaamini beki wao, Shomary Kapombe, ambaye aliumia katika mechi dhidi ya Azam FC, atarejea mapema uwanjani.

# Yanga SC yatamba hesabu zitatimia

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kubanwa ugenini dhidi ya Biashara United, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema bado hesabu zake ni kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga inatarajia kushuka ugenini kesho kuikabili Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Eymael, alisema tayari ameshawaandaa wachezaji wake kutoidharau Kagera Sugar kutokana na ubora wa wachezaji waliokuwa nao na wakifahamu pia hawako kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi.

Eymael alisema anahitaji kufikia malengo yake na amewaandaa wachezaji wake kupambana kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mchezo.

Alisema kila mechi wanayocheza kwao ni muhimu licha ya kuwa tayari bingwa wa msimu ameshapatikana.

"Kuna mchezo dhidi ya Simba mbele yetu, ninajua hilo ila ni lazima tuanze kujipanga na mechi ambayo tuko nayo sasa, ni mchezo mgumu, Kagera Sugar haitakuwa tayari kufungwa kwa mara nyingine," Eymael alisema.

Aliongeza kila mchezaji anajua wanahitaji kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa na ili wafike huko, ni lazima washinde mechi zote zilizobaki.

"Kagera Sugar ni mechi ya ushindani, kwa sababu wanahitaji kulipa kisasi, hawatakuwa tayari kufungwa tena ndani ya siku chache, tutaingia uwanjani tukiwaheshimu wapinzani wetu," Mbelgiji huyo alisisitiza.

Alieleza mbali na ushindani, wanatarajia pia mchezo huo utakuwa na burudani kwa sababu ya ubora wa kiwanja watakachochezea.

"Tunajipanga kumaliza jukumu la kuifunga Kagera Sugar, halafu tuendelee na mikakati ya kuwamaliza Simba, tunahitaji kuchukua kikombe cha FA kuliko

Alisema wanatakiwa kumaliza na Kagere kuhakikisha wanapata alama muhimu ili waendelee na maandalizi ya mechi ya nusu fainali.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042